Sitawahi kukatishwa tamaa katika safari yangu ya Kikristo. Kristo ndani yangu ananifanya nisiyevunjika, nisiyeshindwa, na nifanikiwe katika kila kitu ninachofanya leo!

**MAFUNZO ZAIDI**
Wagalatia 2:20

**MKAKATI WA BIBLIA WA SIKU 365 – SIKU YA 213**
Ayubu 17-19; 1 Wakorintho 2

JUMAPILI , AGOSTI 2




# HEKIMA NI BORA KULIKO RUBI

**Mithali 8:11**
**Kwa maana hekima ni bora kuliko marijani, Na vyote vinavyotamanika havilingani nayo.**

Nimekutana na wanaume na wanawake wengi wenye akili katika miaka yangu ya huduma. Baadhi yao wakiwa na shahada ya uzamivu katika masomo magumu, na wengine wakiwa na sifa zinazotokana na uwezo wao wa ubongo wenye akili nyingi. Na bado wakiwa na akili hii yote, Biblia inafundisha kwamba hekima ni bora zaidi. Kwa nini hii iko hivyo? Kwa sababu hekima ni ufunuo, ni ufahamu wa uhalisia wa ndani wa Ki-Mungu.

Unapotembea katika hekima, huwezi kudanganywa na mifumo ya kidunia; huwezi kuzidiwa na wale wanaotegemea akili ya kidunia. Katika Mwaka huu wa Mafuta ya Ajabu, elewa kwamba Kristo ndiye hekima yako kulingana na 1 Wakorintho 1:30. Hiyo ina maana kwamba hufanyi kazi kama wanadamu wa kawaida; wewe ni wa asili ya kigeni na na bora zaidi kuliko wale walio duniani. Endesha mambo kwa namna hiyo kuanzia sasa!

## MAOMBI YA LEO

Asante, Bwana, kwa kunipa hekima ya Ki-Mungu na kunijaza ufahamu wa kiroho. Kwa sababu hii, ninatembea katika ushindi usio na mwisho katika Jina la Yesu!

## TAMKO LA KINABII

Nikiwa na hekima, naona kile ambacho wengine hawaoni. Utajiri uliofichwa ni wangu, na ufahamu wa afya ya Ki-Mungu ni wangu. Sitapungukiwa au kushindwa na chochote. Utukufu na uwe kwa Mungu!

**MAFUNZO ZAIDI**
1 Wakorintho 2:7-8

**MKAKATI WA BIBLIA WA SIKU 365 – SIKU YA 214**
Ayubu 20-21; 1 Wakorintho 3

GoodNews DAILY

# UMAKINI KWENYE KUABUDU

**Yohana 4:24**
**Mungu ni Roho, nao wamwabuduo yeye imewapasa kumwabudu katika roho na kweli.**

Wakristo wengine wanaposikia neno kuabudu, jambo la kwanza linalokuja akilini ni muziki wa Kikristo wa polepole. Kuabudu ni zaidi ya hayo. Acha nikuonyeshe ufafanuzi.

Kuabudu ni utambuzi na uthamini wa uzuri, baraka, wema, na haki ya Mungu. Unapoabudu, unazungumzia tabia Yake. Kwa mfano, unaposema, "Bwana, wewe ni mzuri; wewe ni mwema," n.k., unafafanua, unatambua, na unathamini tabia Yake.

Mungu anapenda unapomwabudu hivyo kwa sababu inaonyesha Yeye ni nani katika maisha yako; inamtenganisha na kila mtu na kila kitu kingine. Zaidi ya hayo, ibada hutuletea ufunuo mkubwa zaidi wa Mungu. Katika aina hii ya ushirika, anajifunua kwako. Pia anafichua mustakabali wako, maisha yako, na mengine mengi. Waabudu wa kweli hawakosi mwelekeo. Lipe hili umakini zaidi, na litabadilisha maisha yako.

## MAOMBI YA LEO

Mpendwa Bwana, ninatambua na kuthamini uaminifu wako, fadhili, upendo wako, na neema yako inayofanya kazi ndani yangu. Ninakushukuru kutoka kwenye moyo uliojaa ibada katika Jina la Yesu!

## TAMKO LA KINABII

Mwaka huu, ushuhuda wa ajabu na bora utaendelea kuwa sehemu yangu kwa sababu ya moyo wangu wa ibada. Haleluya!

**MAFUNZO ZAIDI**
Wafilipi 3:3

**MKAKATI WA BIBLIA WA SIKU 365 – SIKU YA 215**
Ayubu 22-24; 1 Wakorintho 4

JUMANNE , AGOSTI 4



# MAFURIKO YA MAFUTA YA AJABU

**Isaya 28:21**
**Maana BWANA ataondoka kama vile katika Mlima Perasimu, ataghadhibika kama vile katika bonde la Gibeoni, apate kufanya kazi yake, kazi yake ya ajabu, na kulitimiza tendo lake, tendo lake la ajabu.**

Nikiwauliza watu kama wanaamini Mungu aliumba ulimwengu au alimfufua Yesu kutoka kwa wafu, wengi watakubali bila shaka yoyote. Lakini kwa sababu fulani, linapokuja suala la nguvu halisi inayofanya kazi katika maisha yetu, wengi mara nyingi humtilia shaka.

Waebrania 13:8 inasema, “Yesu Kristo ni yeye yule jana, na leo, na hata milele.” Mungu wa miujiza ya ajabu hajabadilika. Bado ni Mungu anayeshikilia msingi wa dunia, huipa amri asubuhi, na kuweka kila nyota angani usiku. Bado ni Mungu aliyeigawanya Bahari Nyekundu, akasimamisha jua kwenye mhimili wake, na kuwapa vipofu kuona. Kila kazi ya kigeni aliyofanya wakati huo, bado anaifanya sasa.

Jikumbushe hili kila siku na utafurahia mafuta Yake ya ajabu mwaka huu!

## MAOMBI YA LEO

Asante, Baba yangu , kwa kufanya kazi nyuma ya pazia kila wakati kwa niaba yangu ili kutenda kazi za kigeni. Ninashukuru sana katika Jina la Yesu. Amina.

## TAMKO LA KINABII

Kwa mafuta ya ajabu yaliyo juu ya kichwa changu, natamka kila muujiza wangu unapaswa kudhihirika sasa bila kuchelewa!

**MAFUNZO ZAIDI**
Yeremia 32:27

**MKAKATI WA BIBLIA WA SIKU 365 – SIKU YA 216**
Ayubu 25-27; 1 Wakorintho 5

JUMATANO , AGOSTI 5



# NINAWEZA KULIFANYA!

**Luka 9:16-17**
**Akaitwaa ile mikate mitano na wale samaki wawili, akatazama juu mbinguni, akavibariki, akavimega , akawapa wanafunzi wake wawaandikie mkutano. Wakala, wakashiba wote; na katika vile vipande vilivyobakia walikusanya vikapu kumi na viwili.**

Hiki ni mojawapo ya vifungu vyenye nguvu zaidi vya maandiko vinavyoonyesha kile ambacho Mungu anaweza kufanya kwa vitu vichache sana. Ni wangapi wanaosoma haya hivi sasa wanahisi kutostahili, kutokuwa na tumaini, au wanakabiliwa na kazi kubwa mbele ambayo inaonekana ya kutisha sana? Wazo ni kuangalia kile ulicho nacho kupitia macho ya Bwana. Aliangalia mikate mitano na samaki wawili, na akaona vya kutosha kulisha maelfu ya watu.

Unapokabiliana na siku, usimwekee Mungu mipaka. Yeye ni mtaalamu wa kazi za kigeni bila kujali umbo au ukubwa. Sio tu kwamba utashinda, kufanikiwa, na kuongezeka, lakini pia utakuwa na baraka zilizobaki za kushiriki na wengine! Piga kelele, 'Naweza kuyafanya!

## MAOMBI YA LEO

Mungu wangu mpendwa, naleta kila kitu nilicho nacho ili ukitumie. Chochote ninachokabiliana nacho, najua nitafanikiwa kwa sababu nina Wewe.

## TAMKO LA KINABII

Kupitia Kristo, naweza kufanya yasiyowezekana. Ninaweza kukosa kifungua kinywa, chakula cha mchana, au chakula cha jioni, lakini siwezi kukosa uwezo wangu wa mafuta ya ajabu. Haleluya!

**MAFUNZO ZAIDI**
Wafilipi 4:13

**MKAKATI WA BIBLIA WA SIKU 365 – SIKU YA 217**
Ayubu 28-29; 1 Wakorintho 6




# SHAHIDI MAHUSUSI

**Matendo 1:8**
**Lakini mtapokea nguvu, akisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu… hata mwisho wa nchi.**

Maandiko kama haya ni ukumbusho mzuri wa jinsi Baba yetu wa Mbinguni alivyo na upendo. Yesu aliporudi kwa Baba, hakuwaacha watu wake wakiwa hawana nguvu—aliwaachia ahadi thabiti. Hii ilikuwa zaidi ya agizo; ilikuwa wito wa kufikia kusudi la ajabu. Roho yule yule aliyemtia mafuta Yesu ili kuwaletea maskini habari njema, kuwaganga waliovunjika moyo, na kuwaweka huru wafungwa sasa anaishi ndani yetu. Hiyo ina maana kwamba hatubebi habari zake njema tu; tunabeba uwepo wake.

Kwa kujua hili, inapaswa kuwa vigumu kumfanya awe kwa ajili yako peke yako! Acha kila mazungumzo kazini au katika vyumba vya mihadhara yawe fursa kwa Mbingu kugusa Dunia kupitia wewe. Sisi si watazamaji tu katika Ufalme; sisi ni wabeba ufalme, na tunapaswa kuueneza. Kuwa mashahidi wake leo.

## MAOMBI YA LEO

Baba, kwanza kabisa nakushukuru kwa kunipenda sana. Asante kwa kunipa Roho wako Mtakatifu ambaye hunisaidia kuwa shahidi mahususi anayewaelekeza wengine Kwako.

## TAMKO LA KINABII

Maisha yangu ni ushuhuda kamili wa Kristo. Ninapoishi, mimi ni Biblia ya kibiolojia inayotembea, inayozungumza, inayowavuta watu wengi kwa Kristo!

**MAFUNZO ZAIDI**
Warumi 10:13-14

**MKAKATI WA BIBLIA WA SIKU 365 – SIKU YA 218**
Luka 15:1-10; Zaburi 81-83

IJUMAA , AGOSTI 7




# NI YAPI MAONO YAKO?

**Mithali 29:18**
**Pasipo maono, watu huacha kujizuia...**

Nina uhakika umegundua jinsi wakati mwingine katika nyumba zetu, tunavyokuwa na chumba kimoja ambacho hakina kusudi halisi. Chumba hicho huwa chumba cha wageni, au kuhifadhi, au kinyozi, au stoo, au mahali pa kutupia makolokolo yoyote. Hivi ndivyo maisha ya mtu yanavyoweza kuwa ikiwa hakuna kusudi halisi lililoainishwa. Ni rahisi kujaza maisha yako na kila aina ya vitu visivyo na maana vinavyosababisha uharibifu. Maono ni kuhusu kutambua kinachohitaji kubadilika, kutangaza kinachoweza kubadilika, kitakachobadilika, na kusaidia kujielekeza huko. Maono ni kama daraja kati ya mahali ulipo na unapohitaji kwenda.

Ilinibidi niwe na maono ya Spirit Embassy wakati hakukuwa na ishara ya kimwili kwamba ingekuwa hivyo, na matokeo yake tuko hapa leo. Maono ya maisha yako ni yapi? Yaandike na uyafuate kwa makusudi kabisa.

## MAOMBI YA LEO

Baba Mpendwa, nisaidie kuishi maisha ya maono na kusudi linaloongozwa na Roho Wako. Niongoze kuepuka maisha ya kukengeushwa ili niweze kuishi katika utume kwa ajili ya Ufalme Wako katika Jina la Yesu, Amina.

## TAMKO LA KINABII

Sitakosa mwelekeo au kusudi maishani mwangu. Kila hatua ninayochukua imeamriwa na Mungu na husababisha ushuhuda wa ajabu na wa mlipuko katika Jina la Yesu!

**MAFUNZO ZAIDI**
Habakuki 2:2

**MKAKATI WA BIBLIA WA SIKU 365 – SIKU YA 219**
Ayubu 30-31; 1 Wakorintho 7:1-19

JUMAMOSI , AGOSTI 8




GoodNews DAILY

# DIRA KUU

**Zaburi 119:105**
**Neno lako ni taa ya miguu yangu, na mwanga wa njia yangu**

Majaribio yameonyesha kwamba mtu anaweza kutembea katika mstari ulionyooka kwa si zaidi ya mita 100 bila mwanga au sehemu ya marejeleo. Baada ya mita 100, anaanza kuchepuka na kutembea katika miduara.

Hili ndilo somo katika andiko la leo: unapotaka kujua kusudi la Mungu na mwelekeo wake kwenye maisha yako, jifunze Neno la Mungu. Neno ni nuru, ni dira yako; ukilifuata, hutapotea kamwe. Utapita umbali zaidi ya kila kikomo cha “mita 100” ambacho shetani ameweka juu ya maisha yako.

Unapokaa katika Neno, macho yako ya kiroho yatakuwa wazi kwa kile unachopaswa kuona. Utajua la kufanya na kusema katika chumba chochote cha mikutano au chumba cha mahakama. Ingia katika Neno, na hutawahi kukisia kile kilichobaki cha siku yako. Hutashitukizwa na lolote leo.

## MAOMBI YA LEO

Baba Mpendwa, asante kwa zawadi ya Neno Lako, ambalo hutumika kama taa ya kuongoza hatua zangu. Ninaamini kabisa mwongozo Wako na ninafuata Neno Lako kwa bidii katika Jina la Yesu.

## TAMKO LA KINABII

Kuanzia leo, macho yangu yameelekezwa kwenye Neno la Mungu ambalo ndilo dira yangu kuu. Ninachonga njia yangu kuelekea kwenye mipenyo na mafanikio yasiyoisha sasa!

**MAFUNZO ZAIDI**
Mithali 3:5

**MKAKATI WA BIBLIA WA SIKU 365 – SIKU YA 220**
Ayubu 32-33; 1 Wakorintho 7:20-40

JUMAPILI , AGOSTI 9




# DAWA YA MANENO

**Mathayo 12:37**
**Kwa kuwa kwa maneno yako utahesabiwa haki, na kwa maneno yako utahukumiwa.**

Maneno ndiyo nguvu kubwa zaidi Duniani. Sahau umaarufu, utajiri, au hazina zisizohesabika: maneno ndiyo yenye nguvu zaidi. Vita vimeanza kwa sababu ya maneno. Familia zimevunjika; makusanyiko yamekufa, na mataifa yote yanaganda katika umaskini kwa sababu ya maneno.

Mungu aliumba kila kitu kwa maneno na hutegemeza kila kitu kwa maneno. Maneno pia huamua mahali unapoishi milele. Kwa haya yote akilini, umefanya nini kwa maneno? Utatumiaje maneno leo?

Mojawapo ya mambo unayopaswa kufanya ni kusema na mwili wako—kutumia maneno yako ili kuuweka mwili wako katika afya na ukamilifu. Tangaza mara kwa mara kwamba una nguvu na afya kamili. Usemeshe mwili wako, nao utakusikia. Haijalishi daktari alisema nini; tumia maneno ili kurudi kwenye afya. Mwili wa mwanadamu ni kama mnyama anayehitaji kufunzwa. Sisitiza kile unachotaka mwili wako ufanye, na utaanza kukubali maneno yako.

## MAOMBI YA LEO

Asante, Baba, kwa uhai wako unaodunda ndani yangu. Ninatembea katika afya njema na nguvu za Ki-Mungu kwa sababu mimi Nina Wewe.

## TAMKO LA KINABII

Ninaufungua mwili wangu kutoka kwenye kila laana ya udhaifu na kurejesha kila kiungo cha mwili wangu kilichowekwa kwenye madhabahu maovu! Sina magonjwa katika Jina la Yesu!

**MAFUNZO ZAIDI**
Mithali 18:21

**MKAKATI WA BIBLIA WA SIKU 365 – SIKU YA 221**
Ayubu 34-35; 1 Wakorintho 8



# WASAMBAZAJI WA NEEMA

**1 Petro 1:1-2**
**Petro, mtume wa Yesu Kristo, kwa.....kama vile Mungu Baba alivyotangulia kuwajua.....Neema na amani ziongezwe kwenu.**

Jambo moja utakalolipata mara kwa mara katika nyaraka za Paulo, za Petro, na za Yohana pia, ni ufahamu wao wa neema na amani ya Mungu. Walielewa umuhimu na nguvu ya neema na amani katika maisha ya watu wa Mungu. Katika mstari wa leo, Petro anachukua hatua zaidi kutuonyesha jambo la ajabu. Mwanzoni mwa waraka wake, anasema, "...Neema na amani ziongezwe kwenu." Kwa hivyo, neema na amani zinaweza kuongeshwa, lakini vipi?

Mwanzoni mwa waraka wake wa pili, anabainisha jibu: ni kupitia maarifa ya Mungu na Yesu Bwana wetu. Neema iliyozidishwa ina maana ya ubora zaidi, utendaji bora zaidi, kibali, na ustawi katika maisha yako, na inaweza tu kutokea ikiwa unaongeza urafiki wa kweli na Mungu. Sio tu kwamba inakufaidi, lakini wewe, pia, unakuwa msambazaji wa neema kwa kuwapa wengine neema.

## MAOMBI YA LEO

Asante, Baba yangu , kwa neema na amani nyingi ulizonipa kupitia Neno lako.

## TAMKO LA KINABII

Ninapokua katika neema na amani na kuongeza Ufalme wa Baba yangu, hali yangu ya kiroho itapeleka hofu kwenye kambi ya adui. Utukufu!

**MAFUNZO ZAIDI**
Warumi 1:7

**MKAKATI WA BIBLIA WA SIKU 365 – SIKU YA 222**
Ayubu 36-37; 1 Wakorintho 9



GoodNews DAILY

# SAMEHE TU

**Wakolosai 3:13**
**Mkichukuliana, na kusameheana, mtu akiwa na sababu ya kumlaumu mwenzake; kama Baba alivyowasamehe ninyi, vivyo na ninyi.**

Inasikitisha kwamba, jambo gumu zaidi kwa baadhi ya Wakristo kulifanya ni kusamehe. Wamezaliwa mara ya pili, ndimi nyingi, wanatumika kwa uaminifu, waumini wanaosoma Biblia au hata Wachungaji huweka kinyongo kwa miongo kadhaa. Lakini hakuna mahali ambapo Biblia inakuhimiza kushikilia kinyongo au kutosamehe kwa sababu yoyote ile.

Katika mstari wa leo, Paulo anaelezea haswa jinsi unavyopaswa kuwajibu watu wanaokukatisha tamaa au kukukasirisha. Na kwa kuwa maisha yamejaa kukatisha tamaa, ni muhimu kwako kuelewa haswa kile Paulo alichomaanisha alipoandika maneno haya. Kama Mungu angetenda kama watu wengine, na kuchagua kutosamehe, hilo lingekuacha wapi? Kwa makosa yote uliyofanya ambayo Mungu alilazimika kusamehe, kwa nini huwezi kuwapa wengine neema ile ile na kuwasamehe? Hii si kama Kristo. Hakuna haja ya kufikiria; SAMEHE TU!

## MAOMBI YA LEO

Baba Mpendwa, nifundishe kuachilia na makosa niliyotendewa. Safisha moyo wangu dhidi ya chochote nilichokificha moyoni mwangu kwa Roho wako. Asante kwa kunisamehe.

## TAMKO LA KINABII

Sitawahi kushikilia uovu. Hivi sasa, ninamsamehe kila mtu aliyenikosea zamani, sasa, na siku zijazo!

**MAFUNZO ZAIDI**
Mathayo 6:14-15;
Waefeso 4:32

**MKAKATI WA BIBLIA WA SIKU 365 – SIKU YA 223**
Ayubu 38-40; 1 Wakorintho 10:1-17



GoodNews DAILY

# JARIBIO KUBWA

**Luka 16:11**
**Basi, kama hamkuwa waaminifu katika mali ya udhalimu, ni nani atakayewapa amana ya kweli?**

Jinsi unavyosimamia na kuheshimu fedha zako ni jaribio ambalo Mungu hutumia kutathmini kama uko tayari kwa ajili ya viwango vya juu maishani. Anaangalia jinsi unavyosimamia pesa zako, na hilo linamsaidia kuamua kama uko tayari kwa ngazi inayofuata. Je, unaweza kufikiria hilo?

Kwa kumsikiliza Roho wa Mungu na kujidhibiti, unaweza kuishi maisha yasiyo na deni zaidi kuliko jinsi wengine wanavyoishi sasa. Ikiwa tabia zako za matumizi ni mbaya sana kiasi kwamba hutoi zaka na huwezi kutoa kwenye kazi zingine ambazo Roho Mtakatifu anakuhimiza kuziunga mkono, unashindwa mojawapo ya majaribio ambayo Mungu hutumia kubaini kama uko tayari kwa viwango vya juu vya maisha. Pesa zako ndizo mtihani mkubwa! Kuwa msimamizi mzuri wa hilo na uingie katika mambo makubwa zaidi Mwaka huu wa Mafuta ya Ajabu.

## MAOMBI YA LEO

Baba Mpendwa, nifundishe hekima na kujizuia katika masuala ya kifedha, ili uweze kunihesabu kuwa mwaminifu kwa utajiri wa kweli wa Ufalme Wako katika Jina la Yesu.

## TAMKO LA KINABII

Mwaka huu, nitaongezeka kifedha kwa sababu mimi ni msimamizi wa pesa anayeaminika. Deni limefutwa, mauzo yatapanda sana, pesa zinakuja kwa njia za ajabu katika Jina la Yesu!

**MAFUNZO ZAIDI**
Mithali 3:9-10

**MKAKATI WA BIBLIA WA SIKU 365 – SIKU YA 224**
Ayubu 41-42; 1 Wakorintho 10:18-33

ALHAMISI , AGOSTI 13



# KUJISALIMISHA KIKAMILIFU

**Warumi 12:1**
**Basi, ndugu zangu, nawasihi kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana.**

Paulo anatumia lugha ya ajabu katika mstari wetu wa ufunguzi kwa sababu katika nyakati za Agano Jipya, hakukuwa na kitu kama dhabihu iliyo hai linapokuja suala la dhabihu ya wanyama. Wakati mnyama wa kafara alipouawa kwenye madhabahu, hilo lilikuwa ndio mwisho: alikuwa amekufa. Lakini Mungu anatuita tuitoe miili yetu kama dhabihu iliyo hai. Inamaanisha anatafuta watu ambao wanapaswa kujisalimisha kwake kikamilifu, kujitoa kikamilifu kwa kusudi lake, na kuishi kikamilifu kwa ajili yake.

Sio siri kwamba tamaa za mwili wako mara nyingi hupingana moja kwa moja na mpango wa Mungu kwenye maisha yako. Zinapambana kila wakati ili kupata mambo yake. Lakini kumbuka wewe ni nani, dhabihu iliyo hai ambayo Mungu ataweza kufanya kazi nayo ikiwa tu utaitoa iwe hivyo.

## MAOMBI YA LEO

Baba, natubu kwa jinsi nilivyojihusisha na mawazo ya kimwili. Ninahukumu hilo kama uasi, na nakataa kuyapa nafasi kuanzia leo!

## TAMKO LA KINABII

Ninaiharibu kila amana ya kishetani iliyoingia maishani mwangu kwa sababu ya mwili na tamaa mbaya. Kuanzia leo, ninaongozwa na Roho wa Mungu na Yeye pekee!

**MAFUNZO ZAIDI**
1 Wakorintho 6:19-20

**MKAKATI WA BIBLIA WA SIKU 365 – SIKU YA 225**
Luka 15:11-32; Zaburi 84-86

IJUMAA , AGOSTI 14



# TENGA MUDA ‘MARA MOJA’

**Marko 6:45-46**
**Mara akawalazimisha wanafunzi wake wapande mashuani… hata alipokwisha kuagana nao akaenda zake mlimani kuomba.**

Neno “mara” katika mstari wetu ni neno la Kigiriki euthéōs , ambalo linamaanisha kufanya jambo bila kuchelewa au hali yoyote ya kuingilia kati. Neno hili linazungumzia wakati na azimio la Yesu. Mwitikio wake kwa ushindi mkubwa wa kuwalisha watu elfu tano ulikuwa kujiondoa mara moja hadi mahali ambapo angeweza kuomba bila vizuizi.

Kuweka muda wa pekee na Mungu hakupaswi kuwa changamoto kwa watu wanaodai kuwa Wakristo. Bwana Yesu Kristo alikuwa na miaka mitatu tu ya kukamilisha utume Wake, utume mkubwa na wenye harakati nyingi zaidi duniani. Lakini akiwa na haya yote mabegani Mwake, mara kwa mara alitenga muda wa kuomba bila kusumbuliwa. Ni nini kimechukua muda wako kwenye nafasi ya muda wako wa pekee na Mungu? Je, kinafaa? Jibu litakuwa hapana siku zote. Tenga muda kwa ajili ya kile ambacho ni cha milele.

## MAOMBI YA LEO

Baba Mpendwa, kwa uongozi na mafunzo ya Roho Wako Mtakatifu, nifundishe kupangilia siku zangu WEWE ukichukua nafasi ya kwanza.

## TAMKO LA KINABII

Kuanzia leo, kila siku nitakuwa na muda mbele za Baba . Hakuna vikengeushi vitakavyonizuia kuburudishwa na kufanywa upya na Baba yangu katika Jina la Yesu!

**MAFUNZO ZAIDI**
Mathayo 6:6

**MKAKATI WA BIBLIA WA SIKU 365– SIKU YA 226**
Mithali 1-2; 1 Wakorintho 11:1-16



GoodNews DAILY

# ALICHOANZA, ATAKIMALIZA

**Wafilipi 1:6**
**Nami niliaminilo ndilo hili, ya kwamba yeye aliyeanza kazi njema mioyoni mwenu ataimaliza hata siku ya Kristo Yesu.**

Zingatia neno " niliaminilo " katika mstari wa leo. Neno la asili la Kigiriki ni peíthō , ambalo linamaanisha kuwa dhahili, kuwa na uhakika, na kuwa na usadikisho kamili. Mtume Paulo alipoandika barua hii, alikuwa akizungumzia Mungu aliyemjua. Alikuwa amemwona akimtoa katika changamoto za kila aina.

Mwaka huu tulipewa na Mungu kama Mwaka wa Mafuta ya Ajabu. Una uhakika gani kwamba kile alichoanza mwaka huu atakikamilisha? Ukitaka, Roho Mtakatifu anaweza kukamilisha chochote ndani yako. Sharti ni kuwa na imani kubwa ndani Yake kiasi kwamba una uhakika kabisa na una ujasiri kwamba utashuhudia udhihirisho wa kila kazi njema aliyoianza ndani yako.

## MAOMBI YA LEO

Baba, katika Mwaka huu wa Mafuta ya Ajabu, nina hakika kabisa kwamba umefanya kazi kamilifu ndani yangu hadi siku ya Yesu Kristo, nami ninashukuru!

## TAMKO LA KINABII

Natamka kuondolewa kwa kila roho ya udanganyifu inayonizuia kumwamini Bwana. Kila baraka nitakayopewa itatimizwa kikamilifu katika Jina la Yesu!

**MAFUNZO ZAIDI**
1 Wathesalonike 5:24

**MKAKATI WA BIBLIA WA SIKU 365 – SIKU YA 227**
Mithali 3-5; 1 Wakorintho 11:1-16




# TUPA MAVI YA MBWA!

**Wafilipi 3:8**
**...ambaye kwa ajili yake kwa ajili yake nimepata hasara ya mambo yote nikiyahesabu kuwa kama mavi ili nipate Kristo**

Umewahi kukutana na watu ambao hawawezi kuvitupa vitu vya zamani? Magari yaliyoharibika na yaliyojaa panya yameoza uani, huku ndani ya nyumba kukiwa na vitu vingi—rundo la vifaa vya elektroniki vilivyovunjika, mashine za zamani zilizorundikwa ukutani zilizofunikwa na vumbi, na masanduku yaliyojaa nguo zenye ukungu na zilizojaa wadudu. Picha ya kusumbua sana, sivyo?

Maisha ya kiroho ya baadhi ya watu yako hivyo hivyo. Badala ya kushughulikia masuala na kuweka maisha yao safi na wazi, takataka za kiroho huendelea kujikusanya. Mirundikano ya kutosamehe, uchungu, wivu na aina nyingine za takataka za kiroho—yote ni fujo moja kubwa! Unashikilia nini leo? Yote ni mavi ya mbwa! Yatupe kwenye dampo, safisha, na endelea mbele!

## MAOMBI YA LEO

Baba, kwa uongozi wa Roho wako Mtakatifu, nisaidie kutambua ninapoweka vitu vinavyonirudisha nyuma. Sitawahi kushikilia ubaya wowote katika Jina la Yesu!

## TAMKO LA KINABII

Leo, ninaanza mchakato wa kusafisha ili kuondoa kila takataka nilizoshikilia. Nitafanya kazi kwa uhuru na uwazi Mungu anaponitumia katika Mwaka huu wa Mafuta ya Ajabu!

**MAFUNZO ZAIDI**
Wafilipi 3:13-14

**MKAKATI WA BIBLIA WA SIKU 365 – SIKU YA 228**
Mithali 6-7; 1 Wakorintho 11:17-34

## JUMATATU , AGOSTI 17



GoodNews DAILY

# SHUKRANI

**1 Wathesalonike 5:18**
**Shukuruni kwa kila jambo; maana haya ni mapenzi ya Mungu kwenu katika Kristo Yesu.**

Leo, unaposoma haya, huenda usiridhike na mahali ulipo maishani kwa sasa. Kampuni hiyo ya mamilioni ya dola uliyodhani ungekuwa nayo kufikia sasa, jumba hilo la kifahari ulilodhani ungekuwa umejenga, yote bado yapo katika mawazo yako. Hata hivyo, huenda utakubali kwamba mambo si mabaya kama yanavyoweza kuwa! Ukweli ni kwamba, kuna mengi ya kushukuru!

Umefanikiwa kuamka na kufika kanisani leo; baadhi hawajaamka kabisa. Huenda bado hujawa na mamilioni, lakini mshukuru Mungu kwamba una kazi. Huenda bado hujawa na mtoto wako , lakini mshukuru Mungu kwamba una mwenzi wako. Unaona kuna mengi ya kushukuru ukiangalia tu!

Leo, mtu yeyote akikuuliza unaendeleaje, sema tu, “NIMEJAWA SHUKURANI!”

## MAOMBI YA LEO

Baba Mpendwa, ninapofikiria yale uliyonipitisha, na mahali pa amani na pumziko uliponiingiza, naweza kusema tu ASANTE!

## TAMKO LA KINABII

Ninatangaza kwamba sitasahau kamwe kumshukuru Bwana. Ninahama kutoka utumwani hadi uhuru katika kila eneo la maisha yangu kwa sababu shukrani zangu kwa Bwana zitanipa ukuu!

**MAFUNZO ZAIDI**
Waefeso 5:20;
Wakolosai 3:17

**MKAKATI WA BIBLIA WA SIKU 365 – SIKU YA 229**
Mithali 8-9; 1 Wakorintho 12

JUMANNE , AGOSTI 18




# WAFUNDISHE WATOTO

**Kumbukumbu la Torati 11:18-19 (NENO)**
**Yaewekeni haya maneno yangu katika mioyo yenu na akili zenu.... Wafundisheni watoto wenu, yazungumzeni mnapoketi nyumbani na mnapotembea njiani, mnapolala na mnapoamka.**

Wazazi wana jukumu la kuwafundisha watoto wao jinsi ya kuishi kwa ajili ya Mungu na kuwa na ujuzi mzuri wa Neno Lake. Mstari wa leo unawakumbusha wazazi na walezi kutumia kila fursa kufanya hivyo. Baadhi ya wazazi wanafikiri kuwapa watoto wao mahitaji ya kimwili ni jukumu lao kubwa zaidi. Hapana, sivyo! Jukumu lao kubwa zaidi ni kuwafundisha mafundisho na maadili ya Neno la Mungu.

Huenda isiwe katika funzo la Biblia la kila siku, lakini wakumbushe kila mara na wakati wote wema wa Mungu katika maisha yako. Waelezee uumbaji wakiwa njiani kuelekea shuleni. Wakati wa chakula, mthamini Mungu aliyetoa riziki. Mungu yuko kila mahali; waunganishe watoto naye.

## MAOMBI YA LEO

Baba Mpendwa, nifundishe jinsi ya kutumia Neno hili kwa vitendo kila siku ili watoto wangu wakue ndani Yako.

## TAMKO LA KINABII

Watoto wangu watakua na nguvu katika Neno kila siku. Ninatekeleza agizo la kuwaachilia kutoka katika utumwa na ushawishi wowote mbaya unaoathiri ukuaji wao katika Jina la Yesu!

**MAFUNZO ZAIDI**
Mithali 22:6

**MKAKATI WA BIBLIA WA SIKU 365 – SIKU YA 230**
Mithali 10-12; 1 Wakorintho 14:1-19



GoodNews DAILY

# TUKUBALIANE

**Mathayo 18:19**
**Tena nawaambia, ya kwamba wawili wenu watakapopatana duniani katika jambo lolote watakaloliomba, watafanyiwa na Baba yangu aliye mbinguni.**

Wakristo wengi hawatambui nguvu kubwa iliyopo katika makubaliano rahisi. Neno la Kigiriki la "patana" katika mstari wetu mkuu ni neno sumphōnéō . Hapa ndipo neno symphoni linapotoka. Linamaanisha kufanya mapatano, au kufikia makubaliano.

Okestra ya symphoni huchanganya ala nyingi tofauti ili kutoa kito cha muziki. Unaposikiliza mchanganyiko mzuri wa ala, utaelewa ni kwa nini ala moja haingeweza kufanya kazi hiyo. Hakuna mtu anayepaswa kusimama kama kisiwa pekee. Umekusudiwa kushikana mikono na wengine na kukubaliana juu ya mambo, si tu katika maisha yako mwenyewe, bali pia kuhusu mambo yanayogusa dunia. Patana na mtu katika maombi leo kuhusu mfumo wa elimu, mataifa, kanisa lako, familia, n.k., na itakuwa hivyo.

## MAOMBI YA LEO

Baba, asante kwa Neno Lako linaloamuru kwamba pale ambapo umoja unatawala, upako wa uwepo Wako hujaa na kuamuru baraka zako zionekane katikati yetu.

## TAMKO LA KINABII

Ninatabiri kwamba kila ninaposhikana mikono na ndugu kote ulimwenguni katika maombi, kile tunachokiamuru mwilini kitatimia kwa Jina la Yesu!

**MAFUNZO ZAIDI**
1 Yohana 5:14-15

**MKAKATI WA BIBLIA WA SIKU 365 – SIKU YA 231**
Mithali 13-15; 1 Wakorintho 14:20-40

ALHAMISI , AGOSTI 20



# GEUKA

**Ufunuo 2:5**
**Basi kumbuka ni wapi ulikoanguka, ukatubu...**

Neno toba katika tafsiri ya Kigiriki ni neno metanoéō . Linamaanisha kufanya uamuzi , kubadilika kabisa, au kugeuka kabisa katika jinsi mtu anavyofikiri, kuamini, au kuishi. Neno toba linatoa taswira ya mtu anayebadilika kabisa. Tazama Kanisa la Efeso kwa mfano.

Ufunuo 2:5 inatuambia kwamba Bwana Yesu alikuwa na makabiliano ya ana kwa ana na Waefeso alipowaambia kwamba walikuwa wameruhusu uhusiano wao naye upungue. Kutaniko hili hapo awali lilionekana kama kanisa la mfano, mfano kwa makanisa mengine kuangaliazia. Hata hivyo, Yesu alisema washiriki wake na uongozi wake walikuwa “wameanguka”; wote walikuwa wametoweka. Je, ni vivyo hivyo kwako leo? Je, moto uliokuwa nao kwa ajili ya Mungu unawaka kwa ukali zaidi, au moshi pekee ndio uliobaki? Ikiwa ndivyo, kumbuka mahali ulipokosea, tubu, na uwashe tena moto uliokuwa nao kwa ajili ya Mungu kama hapo awali.

## MAOMBI YA LEO

Baba, asante kwa kuniambia kuhusu hitaji langu la kutubu. Kuanzia leo, ninabadilisha jinsi nilivyokuwa nikifikiria na kuishi.

## TAMKO LA KINABII

Ninatabiri kwamba kila kitu kinabadilika maishani mwangu kuanzia sasa. Ninakuza ushirika wenye maana Roho Mtakatifu anaponiwasha kwa ajili ya Mungu katika Jina la Yesu!

**MAFUNZO ZAIDI**
Matendo 3:19

**MKAKATI WA BIBLIA WA SIKU 365 – SIKU YA 232**
Luka 16:1-15; Zaburi 87-88




# NI KIPAUMBELE

**Luka 15:7**
**.....kutakuwa na furaha mbinguni kwa ajili ya mwenye dhambi mmoja atubuye, kuliko kwa ajili ya wenye haki tisini na kenda ambao hawana haja ya kutubu.**

Unapoelewa kweli thamani ya roho, uinjilisti unakuwa zaidi ya idara kanisani; unakuwa utume wako nambari moja. Ukweli tu kwamba bado kuna wengi ambao hawamjui Mungu unapaswa kukutafuna unapowalilia na kuwaombea wokovu wao. Upendo unakusukuma kuzungumza bila aibu na kila mtu aliye na masikio ya kusikia kumhusu.

Unaona, shetani anataka watu wavurugwe na umaarufu, utajiri, na raha ili wasahau umilele. Lakini kama balozi wa Kristo, jukumu lako ni kuwasaidia kuona ukweli. Anza kuona kila roho kama hazina inayosubiri kurudishwa.

Ikiwa Mbingu yote inafurahi kwa ajili ya mwenye dhambi mmoja anayetubu, je, tunapaswa kufanya kazi kwa bidii zaidi kiasi gani ili kuona ikitokea tena na tena ? Fanya wokovu wa roho kuwa kipaumbele!

## MAOMBI YA LEO

Mpendwa Bwana, asante kwa kuokoa maisha yangu na kunileta katika familia yako. Sasa nitumie, Bwana, kuleta roho zaidi zilizopotea katika nuru yako ya milele.

## TAMKO LA KINABII

Kwa Neno hili leo, moyo wangu utawaka kwa huruma kwa waliopotea zaidi ya hapo awali. Nitawatoa wengi kutoka katika himaya ya giza na kuwaingiza katika nuru ya ajabu ya Mungu!

**MAFUNZO ZAIDI**
Yohana 3:16-17

**MKAKATI WA BIBLIA WA SIKU 365 – SIKU YA 233**
Mithali 16-18; 1 Wakorintho 15:1-28



GoodNews DAILY

# MAHUBIRI YENYE SAUTI KUBWA

**Wafilipi 2:15**
**Mpate kuwa wana wa Mungu wasio na lawama, wala udanganyifu, wasio na ila kati ya kizazi chenye ukaidi,kilichopotoka, ambao kati ya hao mnaonekana kuwa kama mianga katika ulimwengu,**

Huwa nasema kila mara kwamba kuhubiri Injili si kusimama tu nyuma ya mimbari, kuvaa suti nzuri na kushikilia kipaza sauti. Mara nyingi, mahubiri yenye sauti kubwa na yenye ufanisi zaidi ni maisha yako. Jinsi unavyoishi, unavyozungumza, na unavyohusiana na wengine inapaswa kuwavuta watu kwa Kristo.

Andiko letu kuu ni ukumbusho kamili wa jinsi unavyopaswa kuenenda katika nyakati hizi hatari ambapo maadili yamepitia dirishani. Dunia imejaa watu mabaradhuli na wapotovu. Waangazie nuru yako katika maisha yao. Watu wanakutazama: marafiki zako, wanafamilia, wafanyakazi wenzako, na hata wageni. Maisha yako ni ujumbe. Waache watu "wasome" maisha yako kama ishara kamili kwa Kristo.

## MAOMBI YA LEO

Mungu mpendwa, nakushukuru kwa kunifanya kuwa barua iliyo hai. Maisha yangu yanaakisi asili yako na kuwatia moyo wengine kukufuata.

## TAMKO LA KINABII

Ninaamuru na kutangaza kwamba kila mtu anayenigusa ataona DNA ya ajabu ya Mungu ndani yangu. Kama Mungu alivyo, ndivyo nilivyo mimi; kwa hivyo, mimi ni mafanikio!

**MAFUNZO ZAIDI**
Mathayo 5:16

**MKAKATI WA BIBLIA WA SIKU 365 – SIKU YA 234**
Mithali 19-21; 1 Wakorintho 15:29-58




# MGENI KAMILI

**Waefeso 2:10**
**Maana tu kazi yake, tuliumbwa katika Kristo Yesu.......**

Kama Wakristo wangeelewa jinsi walivyoumbwa kikamilifu , maombi mengi yangepitwa na wakati. Mungu alikuumba bila aina yoyote ya kasoro, ukomo, au kizuizi. Wewe ni kazi yake bora iliyoumbwa vizuri, kamilifu, bora na timilifu.

Mstari wa leo unasema wewe ni kazi ya mikono Yake. Sio matokeo ya daktari mzuri, vitamini, au utaratibu mzuri wa lishe—wewe ni kazi ya Mungu. Hakuna mwanasayansi katika ulimwengu huu anayeweza kuelewa kikamilifu mashine kamili ambayo ni wewe. Kwa hili kuwa akilini, simama imara dhidi ya hila za shetani. Kataa kuwa mgonjwa, kataa kuwa mshindwa au mwathirika maishani. Tembea katika udhibiti na ukuu juu ya hali za ulimwengu huu. Wewe ni kiumbe wa ajabu wa Mungu, mgeni kamili, mkamilifu katika kila njia!

## MAOMBI YA LEO

Asante, Baba, kwa kunifanya kuwa kazi yako bora kabisa. Kwa sababu umeniumba kikamilifu sana, ninatembea katika mafanikio na ushindi ambao tayari umeniwekea katika Jina la Yesu!

## TAMKO LA KINABII

Ninakataa kuwa mgonjwa au kukata tamaa maishani. Kuanzia leo, ninatembea duniani kama mungu haswa. Ninatawala katika kila uwanja na sitashindwa kamwe. Haleluya!

**MAFUNZO ZAIDI**
Tito 2:14

**MKAKATI WA BIBLIA WA SIKU 365 – SIKU YA 235**
Mithali 22-24; 1 Wakorintho 16



GoodNews DAILY

# ACHA MOTO UWAKE!

**2 Timotheo 1:6**
**Kwa sababu hiyo nakukumbusha, uichochee karama ya Mungu, iliyo ndani yako kwa kuwekewa mikono yangu.**

Katika safari ya Wakristo wengi, bidii waliyokuwa nayo hapo awali kwa mambo ya Mungu huanza kupungua. Binafsi nimekutana na viongozi na watu wa kawaida ambao walifikia hatua ambapo kilichobaki ndani yao ni makaa machache ya moto. Hivi ndivyo nilivyowasaidia.

Katika mstari wa leo, “kuchochea” ni neno la Kigiriki anazōpyréō , ambalo linamaanisha kuamsha tena au kuchochea bidii . Paulo alimhimiza mhudumu huyo mchanga kuongeza kuni kwa makusudi na kwa kuendelea kwenye makaa yanayokufa moyoni mwake.

Labda uko kama Timotheo alivyokuwa: kile ulichohisi hapo awali si kile kilichopo leo. Ninakutia moyo uchukue muda na ubofye kitufe cha kuamsha upya katika mtembeo wako wa kiroho. Anza upya. Una nguvu zote za kuamsha roho yako na kuwasha miali hiyo tena.

## MAOMBI YA LEO

Baba, nawajibika kwa kuruhusu moto ndani yangu ufifie. Kwa Roho wako Mtakatifu, nitaanza upya leo na kuwasha moto upya ili uwake ndani yangu tena.

## TAMKO LA KINABII

Nimfukutwa kwenye moto. Maisha yangu ni maisha ya moto na bidii kwa Mungu! Sitaruhusu moto huo uzime kamwe kwa Jina la Yesu!

**MAFUNZO ZAIDI**
1 Timotheo 4:14

**MKAKATI WA BIBLIA WA SIKU 365 – SIKU YA 236**
Mithali 25-26; 2 Wakorintho 1




**JUMANNE , AGOSTI 25**

# WAFU KWA DHAMBI

**Warumi 6:11**
**Vivyo hivyo, ninyi nayi jihesabuni kuwa wafu kwa dhambi na walio hai kwa Mungu katika Yesu Kristo.**

Nataka uzingatie neno “jihesabuni” katika mstari wa mada wa leo. Katika tafsiri ya Kigiriki, ni neno logízomai , ambalo linamaanisha kuhitimisha au kuhesabu tendo kama tayari limefanywa, linalohitaji uthibitisho na utambuzi wako tu.

Hili ni muhimu sana kwa sababu linakuambia kwamba katika akili ya Mungu, yeyote uliyekuwa hapo awali hana tena dai lolote la wewe ni nani sasa katika Kristo. Dhambi na nguvu yake ya kuchochea imeangamizwa na nguvu ya Msalaba. Thibitisha na utambue hili katika maisha yako. Wewe si yule uliyekuwa hapo awali, haijalishi shetani anakukumbusha mara ngapi. Katika Kristo, mtu huyo wa zamani amekufa. Usitoe nafasi kwa mtazamo wa dhambi; umekufa kabisa!

## MAOMBI YA LEO

Asante, Bwana, kwa wokovu wako ambao ulihakikisha kwamba maisha yangu ya zamani, utu wangu wa zamani, tabia yangu ya zamani inakoma, haleluya!

## TAMKO LA KINABII

Mimi wa zamani nimekufa kitambo. Ninaishi mbali zaidi ya hali kwa sababu hakuna dhambi inayonizuia katika Jina la Yesu!

**MAFUNZO ZAIDI**
Wagalatia 2:20

**MKAKATI WA BIBLIA WA SIKU 365 – SIKU YA 237**
Mithali 27-29; 2 Wakorintho 2



# FAHARI YA KUWA CHUMVI

**Mathayo 5:13**
**Ninyi ni chumvi ya dunia....**

Chumvi ni ya kawaida sana kiasi kwamba unaweza kuipata popote. Lakini katika nyakati za Agano Jipya, chumvi ilikuwa bidhaa ghali na ya thamani ambayo ilihitajika sana katika nyanja nyingi za maisha. Bwana Yesu alipowalinganisha wasikilizaji wake na chumvi, alijua haswa aina ya picha ambazo alitaka kuziangaza akilini mwao, na alijua kwamba mfano huo ungegusa hisia zao.

Chumvi ilitumika kama kikolezi, kihifadhi, dawa ya kuua vijidudu, dawa ya uponyaji, na mengineyo. Sifa hizi zote zinazungumzia wewe unapaswa kuwa nani kama Mkristo. Je, unashawishi ulimwengu wako kwa njia sahihi? Je, watu walio karibu nawe wanahisi athari za chumvi yako ? Chumvi ilipo, matokeo yanafuata. Kuwa uthibitisho!

## MAOMBI YA LEO

Mungu mpendwa, asante kwa kunifanya niwe chumvi hapa Duniani.

## TAMKO LA KINABII

Mimi ni chumvi. Ninaleta uponyaji kwa wagonjwa; Ninaua vijidudu katika maeneo yenye sumu, na kuwapa ladha wale wanaonizunguka. Utukufu kwa Mungu!

**MAFUNZO ZAIDI**
Marko 9:50

**MKAKATI WA BIBLIA WA SIKU 365 – SIKU YA 238**
Mithali 30-31; 2 Wakorintho 3



GoodNews DAILY

# SITADANGANYWA

**Mathayo 24:4**
**..... Angalieni mtu asiwadanganye**

Huna haja ya kutazama ulimwengu unaokuzunguka kwa muda mrefu ili kuona udanganyifu unafanya kazi, hata kutoka sehemu ambazo hutarajii sana. Upotovu wa maadili umeenea sana kiasi kwamba unaweza kuhisi tumefikia hatua ya anguko kuu.

Katika mstari hapo juu, Bwana Yesu alitabiri kwa usahihi udanganyifu huu wa duniani kote katika siku za mwisho na kuwatahadharisha wanafunzi Wake kwamba itakuwa ishara kwamba kurudi Kwake kulikuwa karibu. Tunapokaribia zaidi siku za mwisho za wakati huu, tunahitaji kukumbuka onyo la Kristo kuhusu msimu ambao udanganyifu ungeushika ulimwengu wote. Wakati huo ni sasa. Wakati wa kurudi kwa Bwana umekaribia, ndugu na dada. Kuwa na bidii, kuwa macho, linda moyo wako, na msidanganyike!

## MAOMBI YA LEO

Baba, naomba unipe ujasiri wa ndani wa kusimama imara katika Neno la Mungu na kamwe nisidanganyike katika Jina la Yesu!

## TAMKO LA KINABII

Macho yangu yamepakwa mafuta ya ajabu ambayo hunipa uwezo wa kuona kupitia kila aina ya udanganyifu! Sitadanganywa , Utukufu uwe kwa Mungu!

**MAFUNZO ZAIDI**
2 Wathesalonike 2:3

**MKAKATI WA BIBLIA WA SIKU 365 – SIKU YA 239**
Luka 16:16-31; Zaburi 89-90



IJUMAA , AGOSTI 28

# TAYARI KWA KUPIGANA!

**1 Timotheo 6:12**
**Piga vita vile vizuri vya imani....**

Kuna dhana potofu ya kawaida miongoni mwa Wakristo kwamba wanafikiri ukishazaliwa mara ya pili, hutawahi kukumbana na changamoto yoyote maishani mwako. Hii si kweli hata kidogo. Kutembea kwetu na Bwana ni kutembea kwa imani, na kulingana na mstari wa leo, njia ya imani mara nyingi inahitaji mapambano ili kuikamilisha.

Ukipitia mapambano katika njia ya kuelekea malengo yako, usishangae au kushtuka. Mungu alikuonya mapema kupitia Mtume Paulo kujiandaa kwa ajili ya mapambano. Usikubali au kujisalimisha kwa ndoto zako ulizopewa na Mungu. Simama imara dhidi ya kila upinzani na uvuke kwa ushindi leo!

## MAOMBI YA LEO

Baba Mpendwa, neema ninayohitaji kupigana vita vizuri vya imani iongezwe katika maisha yangu katika Jina la Yesu!

## TAMKO LA KINABII

Roho Mtakatifu ndani yangu anijaza nguvu nyingi zinazozima kila nguvu inayonipinga. Nitasimama imara hata ushindi.

**MAFUNZO ZAIDI**
2 Timotheo 4:7

**MKAKATI WA BIBLIA WA SIKU 365 – SIKU YA 240**
Mhubiri 1-3; 2 Wakorintho 4

JUMAMOSI , AGOSTI 29




# CHINI HADI KWENYE KITU MAHUSUSI

**1 Yohana 5:15 (SRUV)**
**Na kama tukijua kwamba atusikia, tunapoomba chochote, tunajua kwamba tumetimiziwa zile haja tulizomwomba.**

Baadhi ya maombi “hayajibiwi” kwa sababu tu sio mahususi vya kutosha. Acha nikuulize hivi: unapoomba, je, unaomba maombi ya jumla ya baraka, au umejifunza siri ya kuwa mahususi kwa Mungu unapoomba? Maombi kama, “Mungu anibariki maisha yangu yote,” si mahususi vya kutosha. Ni eneo gani hasa unaloomba baraka hii? Aina hiyo ya maombi yasiyoeleweka na ya jumla hayatatoa matokeo yoyote.

Katika mstari wa leo, maneno ‘tunapoomba chochote’ yanamaanisha kutaja mambo mahususi. Tafsiri ya Kigiriki ya neno chochote inamaanisha nani, nini, kipi . Unaona jinsi hilo linavyovutia? Kwa hivyo, unapoomba, taja haswa nani, nini na unachorejelea . Tafuta maandiko yanayounga mkono maombi yako na uwe mahususi!

## MAOMBI YA LEO

Asante, Bwana, kwa kunielekeza kupata ahadi zako mahususi zinazotumika kwa hali mahususi maishani mwangu katika Neno Lako!

## TAMKO LA KINABII

Ninaamuru kwamba ukamilifu wa Mungu umeanzishwa katika kila eneo ambalo nimeomba maishani mwangu. Mafanikio ni yangu!

**MAFUNZO ZAIDI**
Yohana 14:13-14

**MKAKATI WA BIBLIA WA SIKU 365–SIKU YA 241**
Mhubiri 4-6; 2 Wakorintho 5



GoodNews DAILY

# MTUMIAJI ALIYEIDHINISHWA

**Matendo 19:15**
**Yule pepo mchafu akawajibu, akawaambia, Yesu namjua, na Paulo namfahamu; lakini ninyi ni nani?**

Ukiwa ndani ya Kristo, wewe ni mtumiaji aliyeidhinishwa wa Jina la Yesu na nguvu ya Roho Mtakatifu. Pepo mchafu aliyeonyeshwa katika mstari wa leo alijua Jina la Yesu na alimjua Paulo kwa sababu Paulo alikuwa ndani ya Kristo na alikuwa mtumiaji aliyeidhinishwa wa Jina la Yesu!

Kama Mkristo aliyekaliwa na nguvu ya Roho Mtakatifu, una mamlaka yote Mbinguni na Duniani uliyopewa (Mathayo 28:18). Hiyo ina maana kwamba nguvu ile ile ambayo Yesu Kristo anafanya kazi nayo, unayo! Umepewa mamlaka ya kuzungumza kwa niaba ya Yesu na kutumia mamlaka juu ya uwepo wowote mbaya unaokuja leo. Tumia mamlaka yako kufanya kazi za kigeni leo!

## MAOMBI YA LEO

Asante, Baba, kwa kunipa mamlaka ya kutumia Jina la Yesu! Nikiwa na Jina hili lenye nguvu, siwezi kushindwa katika Jina la Yesu!

## TAMKO LA KINABII

Ninatumia nguvu iliyo ndani yangu kufanya kila shambulio baya lililokusudiwa kuniangamiza liwe bure. Sitakuwa aibu kamwe ikiwa tu natumia mamlaka hii!

**MAFUNZO ZAIDI**
Waefeso 1:20-22

**MKAKATI WA BIBLIA WA SIKU 365–SIKU YA 242**
Mhubiri 7-9; 2 Wakorintho 6



GoodNews DAILY

# KUWA MWEMA

**Waefeso 4:32**
**Tena iweni wafadhili ninyi kwa ninyi, wenye huruma , mkasameheane kama na Mungu katika Kristo alivyowasamehe ninyi.**

Neno “wafadhili” kutoka kwa andiko letu kuu ni neno la Kigiriki chrēstós . Linamaanisha kuwa mpole, mkarimu, na mwenye moyo mkunjufu, miongoni mwa mambo mengine. Ukiwa mkarimu, wewe ni mtu ambaye ni mwangalifu na mwenye kujali mahitaji ya wengine.

Neno hili linaelezea mtazamo ambao Bwana Yesu anataka kutuletea kwa nguvu ya Roho Mtakatifu. Kufundisha wema si kwa ajili ya watoto wa chekechea au shule ya Jumapili pekee; hii ni kwa kila mtu aliyepewa jina la Kristo. Bwana Yesu aliguswa na huruma alipomwona mtu mwenye uhitaji. Alikuwa mkarimu. Wakristo wengine ni “kimya” sana kuonyesha wema. Wanafikiri kuwa mkarimu ni udhaifu, lakini Baba yetu mwenyewe ndiye wema. Tunapofunga mwezi huu, hakikisha unasonga mbele na mwaka katika wema kwa wengine!

## MAOMBI YA LEO

Baba, kwa Roho wako, nifundishe jinsi ya kuonyesha wema kwa wale wanaouhitaji zaidi.

## TAMKO LA KINABII

Ninaacha chochote ambacho kimekuwa kikinizuia kuwa mwema kwa wengine. Siku zangu zijazo zitajawa na huruma kwa watu wa Mungu!

**MAFUNZO ZAIDI**
1 Petro 3:8-9

**MKAKATI WA BIBLIA WA SIKU 365 – SIKU YA 243**
Mhubiri 10-12; 2 Wakorintho 7



# MPANGILIO WA MAFUTA

**1 Samweli 10:1, 6**
**Ndipo Samweli akatwaa kichupa cha mafuta, akayamimina kichwani pake, akambusu, akasema, Je, BWANA hakukutia mafuta......... nawe utatabiri pamoja nao, nawe utageuzwa kuwa mtu mwingine.**

Mafuta ya ajabu yanapokujia, mabadiliko si ya hiari, yamehakikishwa. Sauli hakujifanya “mtu bora”; alikuwa mtu mwingine kabisa. Hivyo ndivyo upako unavyofanya. Unakupa nguvu kwa ajili ya kazi yako.

Mwaka huu, hutatarajiwa kutimiza kusudi la Mungu kwa uwezo wa kibinadamu. Mafuta ya ajabu yatatoa kile ambacho nguvu zako haziwezi kutoa. Yatabadilisha mawazo yako na kutoa toleo lako ambalo Mbingu tayari inatambua. Tarajia Roho Mtakatifu akuongezee uwezo wako. Unabadilishwa kuwa mtu ambaye wito wako unahitaji.

## MAOMBI YA LEO

Baba, asante kwa mafuta ya ajabu uliyoyaachilia maishani mwangu. Ninajitoa kikamilifu kwa kazi ya Roho Wako. Acha upako Wako unibadilishe ninapofanya upya akili yangu na kujipatanisha na toleo la Mbingu la yule niliyeitwa kuwa.

## TAMKO LA KINABII

Nimepakwa mafuta kwa ajili ya kazi za ajabu na kazi za kigeni. Ninafanya kazi zaidi ya mipaka ya kibinadamu na ninatembea kwa ujasiri katika utimilifu wa wito wangu leo.

**MAFUNZO ZAIDI**
Matendo 1:8;
2 Wakorintho 3:18

**MKAKATI WA BIBLIA WA SIKU 365 - SIKU YA 244**
Wimbo wa Sulemani 1-3; 2 Wakorintho 8




# UMEZUNGUKWA NA KIBALI

**Zaburi 5:12**
**Kwa maana Wewe utawabariki wenye haki; Bwana, utamzungushia radhi kama ngao.**

Kibali si kitu unachokitembelea; ni kitu kinachokuzunguka. Mungu huweka kibali kama ngao kuzunguka maisha yako ili fursa, mpenyo, na milango iliyo wazi ikupate. Mifumo na watu wanaowanyima wengine lazima waitikie tofauti unapofika.

Hata makosa yanaweza kugeuka kuwa ushuhuda pale kibali kinapofanya kazi. Mwaka huu una shughuli za Mungu zisizo za kawaida, zisizozoeleka, na za ajabu. Sera zitabadilika, watu wataitikia, na hali zitabadilika ili kukufaa. Tembea kwa ujasiri leo; upendeleo hauko mbele yako au nyuma yako. Uko kila mahali ukikuzunguka.

## MAOMBI YA LEO

Baba, asante kwa kunizunguka kwa kibali kama ngao. Asante kwa kutembea ndani yangu leo na kuniweka katika nafasi ya kupata ufikiaji wa Ki-Mungu, fursa zisizo za kawaida, na milango iliyo wazi. Acha kibali chako kinene kwa niaba yangu katika sehemu ambazo sauti yangu haiwezi kufikia. Jina langu litajwe katika vyumba ambavyo sijaingia, na ufanye kila kitu ninachogusa leo kifanikiwe, katika Jina la Yesu.

## TAMKO LA KINABII

Ninaamuru na kutangaza kwamba nitaanzisha biashara, nitanunua mali, na kujenga mahusiano yasiyo ya kawaida. Nimezungukwa na kibali cha ajabu. Popote niendapo leo, milango imefunguka kwangu!

**MAFUNZO ZAIDI**
Luka 2:52

**MKAKATI WA BIBLIA WA SIKU 365 – SIKU YA 245**
Wimbo wa Sulemani 4-5; 2 Wakorintho 9

GoodNews DAILY

# OMBA HEKIMA

**1 Wafalme 3:9**
**Kwa hivyo nipe mimi mtumwa wako moyo wa adili niwahukumu watu wako......**

Mungu hakukosoi kamwe kwa kuomba hekima. Badala yake, anaitoa kwa uhuru na kwa ukarimu. Agizo moja kutoka kwa Mungu linaweza kufanikiwa pale ambapo juhudi za miaka mingi zimeshindwa.

Hekima inakuweka sawa ili ujue la kufanya, wakati wa kulifanya, na jinsi ya kulitekeleza kwa ufanisi. Huko Gibeoni, Sulemani hakuomba ushindi, utajiri, au kuondolewa kwa maadui zake. Aliomba hekima, na hekima ilimweka kupokea kile ambacho hata hakukiomba.

Kazi za ajabu zinahitaji hekima ya ajabu. Mungu anafanya mambo ya ajabu, na mawazo ya kawaida hayawezi kusimamia matokeo ya ajabu. Mungu anapoachilia kazi zisizo za kawaida, Yeye pia hutoa ufahamu unaohitajika ili kuzitekeleza bila mapambano. Alika ufahamu wa Mungu; omba hekima.

## MAOMBI YA LEO

Baba, naomba hekima kutoka juu. Nipe ufahamu zaidi ya uzoefu wangu na uelewa wangu zaidi ya miaka yangu. Niongoze mawazo, maamuzi, na matendo yangu leo ili niweze kuambatana nawe ili kutekeleza kila kazi kwa usahihi na urahisi.

## TAMKO LA KINABII

Ninapokea hekima ya Mungu kwa kila hatua ninayochukua leo. Ninajua la kufanya, wakati wa kulifanya, na jinsi ya kulifanya. Kwa hekima ya Mungu, niko mahali sahihi kwa wakati unaofaa, nikifanya maamuzi sahihi na kuona mafanikio yasiyo ya kawaida.

**MAFUNZO ZAIDI**
Yakobo 1:5

**MKAKATI WA BIBLIA WA SIKU 365 – SIKU YA 246**
Luka 17:1-19; Zaburi 91-93



GoodNews DAILY

# SILAHA YA AMANI

**Isaya 26:3**
**Utamlinda yeye ambaye moyo wake umekutegemea, katika amani kamilifu, kwa kuwa anakutumaini.**

Amani kamili si kutokuwepo kwa migogoro. Ni kifuniko cha ulinzi wa Mungu juu ya akili yako hata wakati migogoro inapokuzunguka. Amani hii humzuia adui kutumia shinikizo kukusukuma nje ya njia.

Mwaka huu, amani si kitu utakachofurahia tu, ni kitu unachobeba. Kadri utambulisho wako kama balozi wa Ufalme unavyozidi kuonekana, mwonekano huo huja na kelele, usumbufu, na mapambano. Lakini amani ndiyo silaha yako.

Kumbuka kwamba umetumwa kwa kazi. Wewe ni balozi, na mabalozi hawawi na wasiwasi kamwe. Wanazungumza kwa niaba ya mataifa, na kujiamini kwao kunatokana na nani wanayemwakilisha. Unawakilisha Mbingu. Acha akili hii iwe ndani yako leo: hakuna wasiwasi, hakuna hofu, hakuna kukurupuka. Fukasi tu. Mungu tayari ametangulia mbele yako. Endelea kuzingatia sauti yake na acha amani ikulinde.

## MAOMBI YA LEO

Baba, asante kwa kufunika amani kamilifu. Acha akili yangu ikae juu yako. Nilinde kutokana na usumbufu. Ninakuamini utaniweka sawa na sauti yako leo.

## TAMKO LA KINABII

Ninaamuru na kutangaza, mataifa yatasikia sauti yangu. Ninatembea kwa amani kamilifu. Sitatikiswa, kukengeushwa, au kupotoshwa katika njia kwa Jina la Yesu.

**MAFUNZO ZAIDI**
Wafilipi 4:6-8

**MKAKATI WA BIBLIA WA SIKU 365 – SIKU YA 247**
Wimbo wa Sulemani 6-8; 2 Wakorintho 10




# MKABIDHI MUNGU MIPANGO YAKO

**Mithali 16:3**
**Mkabidhi Bwana kazi zako, na mawazo yako yatathibitika.**

Unapomkabidhi Mungu mipango yako, unakaribisha akili ya Mungu katika chumba cha kupanga maisha yako. Unapomkabidhi kazi na miradi yako, Yeye huleta muundo kwenye mawazo yaliyotawanyika na kuhakikisha uthabiti kwa kila hatua yako.

Mara nyingi, si ukosefu wa maono unaosababisha mkanganyiko, ni uzito wa kujaribu kuyatatua yote peke yako. Lakini mara tu unapoweka miradi, maamuzi, na majukumu yako mikononi Mwake, unaanza kufikiria wazi zaidi, na hatua inayofuata inakuwa rahisi kuona.

Unashirikiana na Mungu wa ajabu. Anaweka mwelekeo, wakati mahususi, miunganiko, rasilimali, na mkakati ili kile ambacho hapo awali ulihisi kuwa kinakulemea kiwe kimepangiliwa na kufanikiwa. Kabla hujasonga mbele leo, tulia. Lete mipango yako mbele Zake. Mruhusu azungumze ndani yake, avuvie pumzi, na atembee mbele ndani yako..

## MAOMBI YA LEO

Baba, ninakupa kila mpango, mradi, na uamuzi moyoni mwangu. Lete ubaya pale nilipokuwa sijui na mwelekeo pale nilipositasita. Asante kwa kuanzisha hatua zangu leo.

## TAMKO LA KINABII

Ninapoweka mipango yangu kwa Bwana, mawazo yangu huimarika. Hekima ya Mungu huongoza wakati wangu, maamuzi, na mkakati. Kila kitu nilichoweka mkono wangu leo kina matunda. Hii ni siku isiyo na makosa!

**MAFUNZO ZAIDI**
Waefeso 1:11

**MKAKATI WA BIBLIA WA SIKU 365 –**
Isaya 1-2; 2 Wakorintho 11




# PAA

**Waebrania 12:1**
**...Na tuweke kando kila mzigo mzito, na dhambi ile ituzingayo kwa upesi...**

Ndege zimeundwa kuruka, lakini jinsi zinavyopaa juu na umbali zinaoenda hutegemea kile zinachobeba. Ndege nzito hupaa polepole zaidi, hufikia urefu wake bora wa kusafiri baadaye, na huunguza mafuta zaidi ili kufikia umbali ule ule. Mafuta yanapochomwa na uzito unapungua, ndege inaweza kupanda juu na kusonga kwa ufanisi zaidi.

Maisha yako hufanya kazi vivyo hivyo. Nguvu ya Mungu ipo, lakini uzito usio wa lazima huathiri jinsi unavyopaa haraka na jinsi unavyoenda. Baadhi ya uzito ni mazoea. Mengine ni mahusiano, mifumo ya mawazo, au mizigo ya kihisia. Bado unaweza kusonga mbele, lakini kupaa ni polepole na juhudi ni kubwa kuliko inavyohitajika.

Kubeba mzigo wa jana hakutakupeleka kwenye kiwango cha kesho. Amua sasa kwamba hakuna kitakachoingilia kile ambacho Mungu amekuandalia. Achilia chochote kinachokuzuia kupaa kwako, na ufikie kiwango cha roho unachohitaji kufikia kwa hatima. Fikia kimo kikuu!

## MAOMBI YA LEO

Baba, funua na uondoe chochote kinachozuia maendeleo yangu. Nipe neema ya kuacha tabia, mahusiano, na mawazo ambayo hayatumikii tena kusudi lako.

## TAMKO LA KINABII

Ninaachilia kila mzigo usio wa lazima. Hakuna chochote kutoka kwenye maisha yangu ya zamani kitakachoweka kikomo cha maisha yangu ya baadaye. Ninafikia kilele ambacho Mungu ameniandalia.

**MAFUNZO ZAIDI**
Wafilipi 3:13-14

**MKAKATI WA BIBLIA WA SIKU 365 – SIKU YA 249**
Isaya 3-4; 2 Wakorintho 12

GoodNews DAILY

# TUMIA MANENO

**Hosea 14:2**
**Chukueni maneno pamoja nanyi, mkamrudie BWANA…**

Watoto wachanga hulia kwa sababu hawawezi kuongea bado. Wanahisi njaa, usumbufu, hofu, au hitaji la kupewa umakini, lakini bila maneno, kulia kunakuwa njia yao pekee ya mawasiliano.

Kiroho, Maandiko yanaita hali hii nepios , mtoto mchanga katika Kristo. Wakristo Nepios huitikia matatizo kama watoto wachanga: kulia kwa shinikizo, kulia kwa sababu ya fedha, kulia kwa sababu ya upweke au majukumu. Suala si hali hiyo; ni ukosefu wa Neno lililonenwa. Mungu hakuwahi kutuagiza kulia maishani mwetu. Alisema, “Chukueni maneno pamoja nanyi .” Neno la Mungu lina nguvu, hubadilisha mazingira, na huamuru matokeo.

Huu si mwaka wa kulalamika kupitia hali. Huu ni mwaka wa kusema! Chukua maneno katika maombi, siku yako, mwili wako, fedha zako, maamuzi yako, mustakabali wako. Jenga ulimwengu wako kwa yale ambayo Mungu tayari amesema.

## MAOMBI YA LEO

Baba, kifunze kinywa changu kunena Neno Lako ili niweze kukombolewa kutokana na kuchanganyikiwa kimya kimya na athari za kitoto. Ninapozungumza, nisaidie kutawala maneno yangu ili maisha yangu yaakisi nguvu ya kile ambacho tayari umesema.

## TAMKO LA KINABII

Kinywa changu ndicho injini ya mafanikio yangu. Ninalipeleka Neno katika kila hali. Ninaamuru uzima, nguvu, ugavi, na ushindi. Maisha yangu huitikia mamlaka ya Neno, na kila kitu hubadilika ninapotamka!

**MAFUNZO ZAIDI**
2 Petro 1:19

**MKAKATI WA BIBLIA WA SIKU 365 – SIKU YA 250**
Isaya 5-6; 2 Wakorintho 13




# SIFA NGENI

**Wagalatia 4:27**
**Kwa maana imeandikwa, “Furahi, wewe uliye tasa, usiyezaa; paza sauti, ulie, wewe usiye na uchungu...”**

Unapompa mtu zawadi anayoithamini kweli, muitikio wake ni wa haraka. Hawasubiri kuichunguza, kuijaribu, au kuichambua. Wanasifu sana , kukushukuru, kusherehekea, na kuonyesha furaha.

Jinsi tunavyopata baraka za Mungu inahitaji sifa ya ajabu. Kama watu wa imani, hatungoji kuona ndipo kufurahi. Tunaamini tunapokea tunapoomba , si wakati udhihirisho unapoonekana.

Usingoje hadi ahadi iwe mikononi mwako ili kufungua mdomo wako. Fanya mazoezi ya sifa zako sasa. Jionee ukitembea kupitia milango ya biashara yako mpya. Sikia mlio wa ufunguo ukifungua gari lako jipya. Jionee ukisaini mkataba wa mpango huo wa mabilioni ya dola. Jiwazie ukiruka, bila maumivu na umepona kabisa. Sifa mapema huandaa msingi wa kile kinachokuja.

## MAOMBI YA LEO

Baba, sifa zangu ziinuke katika imani. Ninapofurahi kabla ya udhihirisho, milango ifunguke, mikataba itiwe sahihi, na uponyaji ufanyike. Ninakusifu sasa kwa yale ambayo tayari yameshaamuriwa Mbinguni.

## TAMKO LA KINABII

Ninamsifu Mungu kabla ahadi haijadhihirika. Sifa zangu huinuka ili zilingane na ukuu wa kile ambacho Mungu ameniandalia! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Amosi 9:13

**MKAKATI WA BIBLIA WA SIKU 365 – SIKU YA 251**
Isaya 7-9; Wagalatia 1

JUMATANO , SEPTEMBA 9




# SHIKA KWA UANGALIFU

**Zaburi 105:15**
**Msiwaguse masihi wangu...**

Katika siku za kale, uwepo wa Mungu ulibebwa katika chombo halisi, Sanduku. Uza aliponyoosha mkono wake ili kulitegemeza, alipigwa na kufa papo hapo (2 Samweli 6:1-7). Alijifunza kwa njia ngumu kwamba kujaribu kumsaidia Mungu bila maagizo Yake ni jambo hatari. Sanduku halingeweza kuguswa ili mradi tuu kwa sababu Mungu aliishi ndani yake.

Sasa uwepo wa Mungu unakaa ndani yako . Wewe ni sanduku la Mungu. Hiyo ina maana kwamba huwezi kuguswa, kushughulikiwa au kukaribiwa kwa vyovyote vile. Sehemu hatari zaidi ya ukweli huu ni kwamba unaamua ni “mguso” gani unaokubalika.

Siku zako za kusukumwa, kutendewa vibaya au kushughulikiwa bila kujali zimekwisha. Mungu anafanya kazi ya ajabu mwaka huu, na wewe ni mpakwa mafuta wake. Unabeba uwepo wake. Na Mbingu hutekeleza kile unachoruhusu na kile unachokataa.

## MAOMBI YA LEO

Baba, asante kwa uwepo wako ulio ndani yangu. Nifundishe kuheshimu kile ulichotia mafuta na kujiheshimu kama makao yako. Nipe utambuzi wa kutambua kile ninachopaswa kuruhusu na ujasiri wa kukataa kile kinacho fedhehesha uwepo wako maishani mwangu.

## TAMKO LA KINABII

Mimi ni mpakwa mafuta wa Mungu. Siwezi kutendewa vibaya. Kila jaribio la kunigusa, kunizuia au kunipinga linasimamishwa na kuhukumiwa kwa Jina la Yesu!

**MAFUNZO ZAIDI**
2 Timotheo 4:14

**MKAKATI WA BIBLIA WA SIKU 365 – SIKU YA 252**
Isaya 9-10; Wagalatia 2



GoodNews DAILY

# WAFU HAWAONGOPI

**Wagalatia 2:20**
**Nimesulubiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi, bali Kristo yu hai ndani yangu…**

Kuna kitabu kinachoitwa Dead Doctors Don’t Lie . Wazo ni rahisi: unaweza kujifunza mengi kutokana na kile ambacho tayari kimekufa. Kulingana na Maandiko, wewe wa zamani ulisulubiwa pamoja na Kristo, “wewe” uliyeumbwa kwa aibu, hofu, kushindwa na ukomo umekufa.

Wafu hawabishani na ukweli. Hawalalamiki au kupingana na kile Mungu anasema. Kama Mkristo, huishi tena kwa biolojia yako bali kwa maisha ya Kristo. Kwa hivyo, kama kiumbe kipya, kuna mambo ambayo hupaswi kamwe kujidanganya tena. Usiseme kamwe kwamba umekataliwa unapokubaliwa katika Mpendwa. Kataa kujiita dhaifu wakati Roho wa Mungu anaishi ndani yako. Usiseme kamwe kwamba umepungukiwa wakati vitu vyote ni vyako. Acha maneno yako yapatane na kusulubiwa kwako na kufufuka kwako.

## MAOMBI YA LEO

Baba, nakushukuru kwamba maisha yangu ya zamani yalisulubiwa pamoja na Kristo. Acha mawazo, maneno, na matendo yangu yaonyeshe asili yake, haki, na ushindi. Ninachagua kuishi kulingana na mimi nilivyo ndani yako. Amina.

## TAMKO LA KINABII

Mimi wa zamani nimesulubiwa pamoja na Kristo. Sasa ninaishi kwa maisha Yake, ukweli Wake na ushindi Wake. Ninakataa utambulisho wa uongo na nasema tu kile kinachokubaliana na maisha yangu ya ufufuo. Kila uongo umenyamazishwa kwa Jina kuu la Yesu!

**MAFUNZO ZAIDI**
Yohana 1:12-13

**MKAKATI WA BIBLIA WA SIKU 365 – SIKU YA 253**
Luka 17:20-37; Zaburi 94-96




# MAOMBI YANAYOKUPA UMILIKI

**Marko 11:23**
**...... hayo asemayo yametukia, yatakuwa yake.**

Kuna ulimwengu ndani ya Mungu ambapo huombi tena; unamiliki! Kitu kinapokuwa chako katika roho, lugha yako hubadilika kutoka ombi hadi tamko. Huombi kile ambacho tayari kiko mikononi mwako: unatamka kama mmiliki.

Mimi na mke wangu tumefikia mahali ambapo mahitaji hayako tena kwenye fokasi yetu. Kama Maandiko yasemavyo, “tunajitosheleza.” Maombi yetu hayaelekezwi tena kwenye kile tunachohitaji bali kwenye kile ambacho Ufalme unahitaji: mataifa, watu, upanuzi, na maendeleo. Hiyo ndiyo maana ya kumiliki: husogeza maombi hadi ngazi nyingine kabisa.

Mwaka huu, maombi yako yanabadilika. Unaposhikilia kile ambacho Kristo tayari amekuandalia, utajikuta ukizungumza kidogo kutokana na matakwa na zaidi kutokana na mamlaka. Huu ni mwaka unaochukua kile kilicho chako kiroho, kifedha, kimwili na kinabii. Utamiliki mali zako kwa Jina la Yesu!

## MAOMBI YA LEO

Baba, asante kwa mamlaka uliyonipa katika Kristo. Badilisha uelewa wangu kutoka kuomba hadi kumiliki, na unisaidie kunena kutoka kwenye mamlaka, si kutokana na uhaba, katika Jina la Yesu.

## TAMKO LA KINABII

Ninamiliki kile ambacho Mungu amenipa. Nachukua mamlaka; siombi. Naamuru ongezeko, utoshelevu na maendeleo ya ajabu katika kila eneo la maisha yangu!

**MAFUNZO ZAIDI**
1 Wakorintho 3:21;
2 Wakorintho 9:8 (AMPC)

**MKAKATI WA BIBLIA WA SIKU 365 – SIKU YA 254**
Isaya 11-13; Wagalatia 3



GoodNews DAILY

# MAOMBI YA AJABU

**Zaburi 5:3**
**BWANA, asubuhi utaisikia sauti yangu, Asubuhi nitakupangia dua yangu na kutazamia.**

Moto wa mafuta ni miongoni mwa hatari zaidi kwa sababu ni ngumu kuuzuia. Mara tu unapowashwa, huwaka moto zaidi, huenea haraka na hukataa kuzimwa kwa njia za kawaida. Moto huruka kutoka ukuta hadi ukuta, ukisafiri, ukiongezeka na kuongezeka. Hii ni picha ya maisha ya maombi yanayowaka

Unapoweka vipande vya maisha yako kwenye madhabahu ya Mungu, moto hushika. Maombi huwaka, na yanaweza kuwasha chochote kinachogusa. “Hatari” ile ile ya moto wa asili wa mafuta inakuwa faida yako: endelevu, isiyoweza kuzuilika, inayosonga haraka, na isiyowezekana kwa adui kuizima.

Katika Mwaka huu wa Mafuta ya Ajabu, maisha yako ya maombi yatawaka. Sio aina dhaifu, ya kawaida ya maombi ambayo hufifia na kufa, bali aina inayoenea katika nyumba yako, maamuzi, fedha na kazi zako. Maombi ambayo huvuta kila eneo lililotawanyika la maisha yako mahali pamoja mbele za Mungu na kuyachoma.

## MAOMBI YA LEO

Baba, acha moto mtakatifu ushuke na uwashe maisha yangu ya maombi kwa mafuta ya ajabu. Choma usumbufu, udhaifu, na kudumaa. Fanya maombi yangu kuwa endelevu, yasiyoweza kuzuilika, na yasiyowezekana kwa adui kuzima.

## TAMKO LA KINABII

Ninapoweka maisha yangu madhabahuni, na moto wa Mungu unateketeza kila sehemu yangu, Mbingu huitikia na kuzimu hupatwa na hofu. Maombi yangu ni hatari!

**MAFUNZO ZAIDI**
Marko 1:35

**MKAKATI WA BIBLIA WA SIKU 365 – SIKU YA 255**
Isaya 14-16; Wagalatia 4




JUMAPILI , SEPTEMBA 13

# KISICHO NA KAZI

**2 Timotheo 1:10**
**Na sasa inadhihirishwa kwa kufunuliwa kwake Mwokozi wetu Kristo Yesu, aliyebatili mauti.....**

Mstari huu unapaswa kuwa mojawapo ya mistari yenye utata zaidi katika Maandiko, lakini sivyo, kwa sababu Wakristo wengi wanakataa kukubali uwezekano mtukufu unaoufichua. Kutokufa si kwa ajili ya mbinguni tu; ni kwa sasa. Na sababu iko wazi: Kristo aliondoa kifo.

Katika Ufalme wetu, kifo kimefutwa . Neno hilo ni katargéō kwa Kigiriki, ambalo linamaanisha kuwa lilifanywa kuwa hakina maana kabisa, hakina kazi, hakiwezi kufanya kazi na hakifanyi kazi. Haleluya! Kifo kimeondolewa nguvu, uweza, na ushawishi wake. Hakipaswi kamwe kutumika, kuwa hai, au kufanya kazi katika maisha ya Mkristo. Ni kinyume cha sheria!

Thubutu kutembea katika nuru ya ukweli huu. Tafakari juu yake hadi iwe sehemu ya maarifa yako, mambo yasiyoweza kujadiliwa. Acha ibadilishe jinsi unavyofikiri, unavyosema, na unavyoitikia hofu, magonjwa, na vikwazo. Kristo hakusimamia kifo. Alikibomoa bomoa. Huwezi kuuawa.

## MAOMBI YA LEO

Baba, asante kwa kazi iliyokamilika ya Kristo. Asante kwa kuwa kifo kimefutwa, kimefanywa kuwa kisicho na nguvu, na hakifanyi kazi maishani mwangu. Acha ufunuo huu ukae ndani kabisa ya roho yangu.

## TAMKO LA KINABII

Sheria ya Roho wa Uzima iko hai na inafanya kazi maishani mwangu. Kifo hakina mamlaka juu yangu. Ninafuta kila jukumu la kifo! Kifo, umefukuzwa kazi!

**MAFUNZO ZAIDI**
Waebrania 2:14-15;
Warumi 8:1-2

**MKAKATI WA BIBLIA WA SIKU 365 – SIKU YA 256**
Isaya 17-19; Wagalatia 5

JUMATATU, SEPTEMBA 14



# BWANA ATAINUKA

**Isaya 28:21**
**BWANA atainuka kama alivyofanya kwenye Mlima Perasimu...**

Bwana anapoinuka, kila kitu hubadilika. Katika Maandiko yote, kuinuka kwake ni ishara ya hatua ya uamuzi. Anapoinuka, hukumu huachiliwa, rehema humiminwa, na kile kilichoonekana kukwama hapo awali huanza kujongea. Anainuka wakati kuchelewa hakuwezi kuendelea tena. Anainuka kutenda kwa niaba ya watu wake, kuwapendelea ili utukufu wake uonekane katika maisha yao.

Katika Mlima Perasimu, Bwana aliinuka ghafla na kuvunja kama mafuriko. Isaya anaiita “kazi Yake ya ajabu,” jambo lisilotarajiwa ambalo lilimshtua kila mtu. Mungu anapoinuka, anachofanya kitakushangaza. Haitakuwa ya hila au ya taratibu. Itakuwa ya haraka, isiyopingika, na kwa wakati unaofaa.

Kila adui wa maendeleo yako, iwe ni shinikizo la kifedha, ugonjwa unaoendelea, milango iliyofungwa, upinzani wa kiroho, au miduara ya kuchelewa, inakabiliwa. Kile kilichokuwa kinapigana nawe kimya kimya kitaanguka kwa mshindo mkubwa. Hakuna kinachoweza kumzuia.

## MAOMBI YA LEO

Baba, asante kwa kusimama kwa niaba yangu. Acha kila kitu kinachosimama dhidi ya afya yangu, fedha, na kazi yangu kiporomoke chini ya uwezo wako. Acha hii iwe siku ambayo kazi yako ya ajabu anapenya kwa ajili yangu.

## TAMKO LA KINABII

Bwana ameinuka kwa ajili yangu! Kilichonipinga kinaanguka. Kila kuchelewa, miduara hasi, na upinzani uliofichika kunahukumiwa. Kazi yake ya ajabu iko katika mwendo!

**MAFUNZO ZAIDI**
Zaburi 68:1-4

**MKAKATI WA BIBLIA WA SIKU 365 – SIKU YA 257**
Isaya 20-22; Wagalatia 6

GoodNews DAILY

# PESA ZA HABARI NJEMA

**Marko 16:15**
**Akawaambia, Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe.**

Inaweza kukushangaza kujua kwamba Wakristo wengi, ingawa wamezaliwa mara ya pili, hawajawahi kusikia Injili. Injili ( euagellion ) ni habari ambayo ni nzuri sana kuwa kweli. Ndugu na dada, ikiwa si habari njema, si Injili.

Injili imekusudiwa kuhubiriwa kila mahali, si kwa watu tu, bali "kwa kila kiumbe." Mara ya mwisho ulipohubiria biashara yako ilikuwa lini? Unaweza kuwa unahudumu kila Jumapili, lakini je, umehubiri habari njema kwenye akaunti yako ya benki?

Acha leo iwe alama ya uzinduzi au kuzindua upya huduma yako ya kuhubiri Injili. Ihubiri kwa kila kiumbe, kila kitu kilichoumbwa. Habari njema kila mahali!

## MAOMBI YA LEO

Baba, nisaidie kuhubiri habari njema hii kwa ujasiri na bila kikomo. Riziki, ongezeko, na upaji viweze kutumikia maendeleo ya Injili katika maisha yangu yote, kwa ajili ya utukufu wako. Amina.

## TAMKO LA KINABII

Ninaamuru na kutangaza: pesa inanitafuta. Sitakosa pesa mwaka huu. Akaunti ya benki, sarafu kutoka mataifa yote zinanijia! Biashara, inastawi zaidi kuliko hapo awali ukiwa na mkondo usioisha wa wateja bora! Fedha, inaongezeka kwa Utukufu wa Mungu. Ninazihubiria pesa zangu: Habari njema kwako!

**MAFUNZO ZAIDI**
Yeremia 22:29

**MKAKATI WA BIBLIA WA SIKU 365 – SIKU YA 258**
Isaya 23-25; Waefeso 1




# URAIBU WA ONGEZEKO

**Mathayo 6:33**
**Bali utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake; na hayo yote mtazidishiwa.**

Watu walio na uraibu wana mifumo. Hupanga siku zao kulingana na kile wanachotamani. Wanavifikiria, wanavipangia, wanavifuatilia, na kujitoa kwa ajili ya hivyo. Yesu alitumia picha hii hii aliposema utafute kwanza Ufalme. "Tafuta" ( epizēteō ) inamaanisha kutafuta au kutamani kwa kipaumbele; ni nguvu inayokataa kukataliwa.

Hebu fikiria kama utafutaji wako wa Mungu ungekuwa na kiwango hicho cha umakini. Kama mtu angechunguza tabia zako, jinsi unavyofikiri, unavyopanga, na unavyotumia muda wako, je, angehitimisha kwamba wewe ni "mraibu" wa mambo ya Mungu?

Pale Mungu anachotaka kinapokuwa kipaumbele chako, unachohitaji huongezwa bila mapambano au kujichosha. Achana na utamaduni wa shughuli nyingi. Jitoe kikamilifu kwenye ajenda Yake. Huu ndio uraibu pekee ambao Mungu ataufadhili.

## MAOMBI YA LEO

Baba, pangilia upya matamanio yangu na urekebishe mwelekeo wangu. Nifundishe kukutafuta kwa nguvu, kipaumbele, na kujitoa. Vunja kila tamaa isiyo mahali pake ili ibadilishane na njaa ya Ufalme Wako na haki Yako.

## TAMKO LA KINABII

Maisha yangu yamejikita kwenye kumfuata Mungu kwa umakini. Ninatamani uwepo wake. Ninajitoa kikamilifu kwa ajenda yake. Mimi ni mraibu wa Ufalme; kila kitu ninachohitaji kinaongezwa, na ongezeko limehakikishwa!

**MAFUNZO ZAIDI**
Mithali 23:4 (MSG); Wafilipi 4:19

**MKAKATI WA BIBLIA WA SIKU 365 – SIKU YA 259**
Isaya 26-27; Waefeso 2



GoodNews DAILY

# KUPINDUA MEZA

**Mathayo 2:20**
**...Kwa maana wamekufa walioitafuta roho ya mtoto.**

Kusudi huvutia upinzani. Kabla ya Yesu kusema neno au kufanya hata muujiza, adui alilenga maisha Yake. Upinzani mara nyingi hujitokeza mapema hatima inapokuwepo. Jibu la Mungu halikuwa mapambano mwanzoni bali uhifadhi: kimbia!

Maandiko yanaonyesha kwamba kukimbia kunaweza kuwa mkakati wa imani. Katika nyumba ya Potifa, Yusufu alikimbia uasherati ili kuhifadhi utakatifu. Daudi alimkimbia Sauli ili kudumisha wito. Paulo alishushwa kwenye kikapu ili kuepuka hatari na kuishi kuhubiri siku nyingine.

Yusufu, mume wa Mariamu, aliagizwa kukimbia ili kuokoa maisha ya mtoto mdogo. Lakini inakuja wakati ambapo Mungu anatangaza, “Wale waliotafuta uhai wako wamekufa.” Msimu unabadilika, na adui aliyekufuata hapo awali ndiye anayefukuzwa. Mungu wa Majeshi ya Malaika anakupigania. Acha kukimbia na usonge mbele. Sasa ni zamu ya adui kukimbia!

## MAOMBI YA LEO

Baba, asante kwa kuhifadhi maisha yangu na hatima yangu katika kila msimu wa upinzani. Nipe utambuzi wa kujua wakati wa kukimbia na hekima ya kujua wakati wa kusonga mbele. Asante kwa kunipigania na kuchakaza kila tishio dhidi ya wito wangu.

## TAMKO LA KINABII

Ninaamuru na kutangaza: kila adui wa hatima yangu amedhoofika. Mungu ananiunga mkono kwa mkono wake wa haki!

**MAFUNZO ZAIDI**
Isaya 41:11-13

**MKAKATI WA BIBLIA WA SIKU 365 – SIKU YA 260**
Luka 18:1-17; Zaburi 97-99



GoodNews DAILY

# UTARATIBU WA MAFUTA

**Zaburi 133:2**
**Ni kama mafuta mazuri kichwani, Yashukayo ndevuni, ndevu za Haruni, Yashukayo mpaka upindo wa mavazi yake.**

Samaki wengi huogelea juu ya mto, lakini inahitaji juhudi zaidi kwenye mtiririko wa maji. Kila kitu kinakuwa kigumu zaidi, maendeleo ni pole pole, nishati hupungua, na upinzani ni wa kudumu. Uzoefu wa maisha ni ule ule hata wakati heshima inapokosekana. Ni kama kujaribu kuruka kutoka ardhini huku umesimama kwa kichwa chako.

Upako huongeza uthabiti pale ambapo kwa kawaida kungekuwa na msuguano; unafanya zaidi kwa jitihada kidogo. Hata hivyo, Mungu alibuni upako utiririke kwa utaratibu maalum: unaanza kichwani ndipo utiririke chini.

Unapowatambua na kuwapa heshima wale ambao Mungu amewaweka juu yako, utakuwa katika nafasi nzuri ya kupokea mafuta. Upako unaouheshimu ndio upako unaouvutia kwako.

## MAOMBI YA LEO

Baba, asante kwa utaratibu uliouweka kwa ajili ya mtiririko wa upako wako. Nisaidie kutambua na kuthamini neema uliyoiweka kwa wengine na kuiheshimu neema hiyo.

## TAMKO LA KINABII

Ninatembea katika utaratibu na heshima ya Ki-Mungu. Ninapotambua na kuthamini wale ambao Mungu amewaweka juu yangu, mafuta hutiririka kwa uhuru katika maisha yangu. Ninapokea yote ambayo upako unatoa, katika Jina la Yesu.

**MAFUNZO ZAIDI**
Waebrania 7:7

**MKAKATI WA BIBLIA WA SIKU 365 – SIKU YA 261**
Isaya 28-29; Waefeso 3

JUMAMOSI, SEPTEMBA 19



# KIBALI KISICHOEPUKIKA

**Isaya 60:2**
**... Bali BWANA atakuzukia wewe, na utukufu wake utaonekana juu yako.**

Hebu fikiria ukiingia kwenye chumba na hali ya hewa inabadilika. Mazungumzo yanasimama. Vichwa vinageuka. Watu wananong’ona, “ Ni nani huyo ?” Hujasema neno lolote, lakini kuna kitu kukuhusu kinachovutia umakini. Watu wanakupa nafasi; wanakupa viti vyao, si kwa sababu wanajua jina lako, bali kwa sababu ya uwepo wako.

Hivyo ndivyo neema inavyofanya. Inakutenga bila kuhitaji utangulizi. Kuna upako wa ajabu maishani mwako unaobadilisha jinsi vyumba vinavyokuitikia. Hapo awali, huenda ulipuuzwa au kubezwa. Mwaka huu, hilo haliwezekani tena.

Hutaingia tu kwenye vyumba; utaviamuru. Utapewa fursa ambazo hazikuwa hata kwenye rada yako. Watu watakukubali bila kujua ni kwa nini. Usiulize. Usipunguze umuhimu wake. Usiombe msamaha. Uliwekwa alama kwa hili.

## MAOMBI YA LEO

Baba, asante kwa utukufu unaokaa juu yangu. Acha kila chumba ninachoingia kiitikie uwepo wangu. Kibali kinifungulie milango ifunguke na kunifanya nitambulike bila maelezo.

## TAMKO LA KINABII

Nina kibali kisichopingika. Hata kwenye ukimya, naonekana. Sifukuzii; naamuru. Utukufu wa Bwana unaonekana juu yangu, na mafuta ya ajabu hunena popote ninapoenda.

**MAFUNZO ZAIDI**
Danieli 1:9;
Isaya 60:1-2

**MKAKATI WA BIBLIA WA SIKU 365 – SIKU YA 262**
Isaya 30-31; Waefeso 4



# NJE YA DUNIANI HII

**Yohana 17:14**
**... Wao si wa ulimwengu, kama mimi nisivyo wa ulimwengu.**

Watu wanavutiwa na matukio ya UFO kwa sababu yanaonekana kufanya kazi kwa sheria ambazo hazilingani na tunachoelewa. Wanasonga tofauti, wanafika bila kutarajia, na kuwaacha watazamaji wakitafuta maelezo.

Taharuki hiyo hiyo ilimfuata Yesu. Alipowaponya wagonjwa na kufanya miujiza, watu walisema hawajawahi kuona kitu kama hicho hapo awali. Matendo yake hayakufuata mifumo iliyozoeleka. Ilikuwa ya nje ya ulimwengu huu.

Kanuni hiyo hiyo inatumika kwako. Jinsi unavyofanya biashara itaonekana kuwa ya ajabu. Jinsi unavyopata pesa haitaendana na hali ilivyo. Jinsi wateja wanavyokupata, milango inavyofunguka kwako, na mahitaji yanapokujia itawafanya wengine kusimama na kusema, “Hatujawahi kuona ikifanywa hivi.” Unabeba utaratibu mwingine, mgao mwingine, njia nyingine ya kuzalisha matokeo. Uko nje ya ulimwengu huu!

## MAOMBI YA LEO

Baba, fanya kazi yangu, riziki yangu, na maendeleo yangu yatendeke zaidi ya mifumo ya kibinadamu, ili utukufu wako uonekane wazi katika maisha yangu. Ninapokea neema ya kufanya kazi kutoka katika ulimwengu mwingine na kutoa matokeo ambayo yanaweza kuelezewa na Wewe pekee.

## TAMKO LA KINABII

Ninafanya kazi kutoka kwenye kiwango cha juu zaidi. Matokeo yangu yanashuhudia kwamba mimi si wa ulimwengu huu. Kila kitu kuhusu maisha yangu ni cha ajabu!

**MAFUNZO ZAIDI**
Marko 2:12 (NKJV)

**MKAKATI WA BIBLIA WA SIKU 365 – SIKU YA 263**
Isaya 32-33; Waefeso 5:1-16

**JUMATATU, SEPTEMBA 21**



GoodNews DAILY

# KUBWA ZAIDI!

**Luka 5:4**
**...... Tweka mpaka kilindini, mkashushe nyavu zenu mvue samaki.**

Googol ni 1 ikifuatiwa na masifuri 100. Googolpleksi ni 1 ikifuatiwa na sifuri za googol. Zaidi ya hayo, wanahisabati hufanya kazi na nambari kubwa sana kiasi kwamba zinaweza kuelezewa tu kwa kutumia nukuu za hisabati. “Nambari yoyote kubwa zaidi” tunayozungumzia ni mahali petu pa kusimama .

Tuna akili ya Kristo, akili isiyojua mapungufu. Kwa hivyo, ingawa idadi ndogo inaweza kuhisi salama, Mungu hakuwahi kuwaagiza watu wake wafikirie kuwa wadogo. Yesu alimwambia Petro atupe nyavu zake kwenye kilindi , si kwenye kina kifupi, na matokeo yake yalikuwa kufurika hadi kufikia hatua ya kuchanika.

Usiogope idadi kubwa. Jiambie dola $10,000 ni chenji isiyo na malipo. Dola $2,000,000 ni pesa ya chakula cha mchana. Dola $1,000,000,000 ni mshahara wako wa chini kabisa. Tumia imani kuanza kutoka hapo ulipo hadi kwenye maji ya kina kirefu. Usisimame hadi utakapohitaji kujipatia jina la kuelezea jinsi ulivyofanikiwa.

## MAOMBI YA LEO

Baba, panua maono yangu na utawanye kila hofu inayohusiana na kuongezeka. Nifundishe kufikiria kwa kina zaidi na sio kudharau uwezo wako wa kunifanikisha.

## TAMKO LA KINABII

Nitatangaza idadi inayoakisi ukuu wa Mungu ninayemtumikia. Huu ni mwaka wangu wa kutweka ndani ya vilindi; Mungu hujaza nyavu zangu hadi zitakapopasuka.

**MAFUNZO ZAIDI**
1 Wakorintho 2:16

**MKAKATI WA BIBLIA WA SIKU 365 – SIKU YA 264**
Isaya 34-36; Waefeso 5:17-33




# MAISHA YA AJABU

**Luka 2:26**
**Naye alikuwa ameonywa na Roho Mtakatifu ya kwamba hataona mauti kabla ya kumwona Kristo wa Bwana.**

Una uzima ule ule alio nao Mungu; ni uhalisia wa sasa. Yohana 3:16 inasema kwamba yeyote amwaminiye Kristo asipotee bali awe na uzima wa milele. Kiumbe kipya katika Kristo hakikusudiwi kuishi chini ya matarajio ya kifo. Lazima uwe na zōé, uzima kama Mungu alio nao, sasa.

Simeoni alipokea ufunuo kutoka kwa Roho Mtakatifu kwamba hangeona mauti hadi amwone Masihi. Lakini una ufunuo zaidi ya Simeoni: Roho atoaye uzima sasa anaishi ndani yako. Warumi inatuambia kwamba Roho yule yule aliyemfufua Kristo kutoka kwa wafu huhuisha mwili wako unaokufa, akiendelea kutoa uzima, nguvu, na kuzaliwa upya kwa mwili wako wa nyama.

Amua kwamba hutakufa. Amua. Amini. Jiambie, "Nitakuwa hai na mzima mpaka Bwana atakapokuja." Ishi !

## MAOMBI YA LEO

Baba, asante kwa uzima wako ndani yangu. Leo ninakabidhi viungo vyangu kwa Roho atoaye uzima ili niweze kuona uzima wa milele ukitenda kazi ndani yangu sasa.

## TAMKO LA KINABII

Nina uzima wa Mungu ndani yangu. Sitakufa. Ninaamuru na kutangaza kwamba nitakuwa hai na mzima Bwana atakaporudi.

**MAFUNZO ZAIDI**
1 Wakorintho 15:51

**MKAKATI WA BIBLIA WA SIKU 365 – SIKU YA 265**
Isaya 37-38; Waefeso 6




# BIMA YA MAISHA

**2 Wakorintho 9:7**
**Kila mtu na atende kama alivyokusudia moyoni mwake ....... kwa maana Mungu humpenda yeye atoaye kwa moyo mkunjufu.**

Watu hununua bima ya maisha ili kutoa ulinzi, riziki, au usalama kwa wapendwa wao watakaowaacha. Lakini katika Ufalme, kuna aina nyingine ya bima ya maisha, inayokuhifadhi . Unapokuwa mtoaji mkarimu na mwenye haraka ya kufanya hivyo, unaanzisha sera ya bima ya maisha ya Mungu isiyo ya kawaida.

Dorkasi alikuwa mwanamke katika Biblia ambaye alifufuliwa kwa sababu ya kutoa kwake daima. Sadaka zake zilizungumza kwa niaba yake hata wakati ambapo hakuweza, na Mungu alihifadhi uhai wa mtoaji wake.

Linda bima yako ya maisha kwa kuwa aina ya mtoaji ambaye Mungu anamtafuta; si mtu anayetoa kwa kushinikizwa, bali mtu anayetoa kwa matarajio ya furaha, akijua kwamba anatimiza matakwa ya moyo wa Mungu.

## MAOMBI YA LEO

Baba, nakushukuru kwa neema ya kuitikia mwaliko wako wa kutoa kwa haraka na kwa hiari. Furaha yangu kubwa iwe kukufurahisha katika yote ninayofanya.

## TAMKO LA KINABII

Mimi ni mtoaji wa Mungu mchangamfu na mwenye haraka! Ninapotoa, ninajihakikishia mfumo wa ulinzi wa Mungu juu ya maisha yangu, afya yangu, familia yangu, na hatima yangu. Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Matendo 9:36-41

**MKAKATI WA BIBLIA WA SIKU 365 – SIKU YA 266**
Isaya 39-40; Wafilipi 1

ALHAMISI, SEPTEMBA 24




# KAZI YA AJABU, MAJUKUMU YA KIGENI

**Yohana 10:34**
**Yesu akawajibu, Je! Haikuandikwa katika torati yenu ya kwamba, Mimi nimesema, Ndinyi miungu?**

Tumeumbwa kwa mfano na sura ya Mungu. Hiyo ina maana kwamba tunafanana si tu na asili yake, bali pia na jinsi anavyofanya kazi. Isaya anatuambia kwamba Bwana hufanya kazi yake ya ajabu na majukumu yake ya kigeni . Ikiwa kazi za Mungu ni za ajabu na za kigeni, kama zile zilizofanywa kwa mfano wake, na zetu zinapaswa kuwa za ajabu pia.

Kuzivuna roho ili kuziandaa kuondoka katika sayari hii ni kazi ya ajabu. Kupanga kwa ajili ya umilele huku ulimwengu ukifukuzia mitindo ni kazi ya kigeni. Kupanda sadaka katika Ufalme ili mataifa yaweze kuvunwa kwa siku moja ni jambo la ajabu.

Unabeba DNA ya Mungu ambaye njia zake huingilia kanuni na kupinga mifumo. Wakati utii wako unaonekana usio wa kawaida, au wakati kazi yako inapoonekana kuwa nje ya mstari wa ulimwengu, kumbuka hivi ndivyo ulivyo. Uliumbwa kwa ajili ya kazi ambayo haiwezi kuelezewa bila Mungu.

## MAOMBI YA LEO

Baba, niokoe kutoka kwa uraibu wa kutaka kukubalika, na unitie nguvu ili kutekeleza majukumu yanayokatiza kanuni na kupinga mitindo. Acha niwe shahidi safi kwamba unafanya kazi Yako ya ajabu kupitia mimi.

## TAMKO LA KINABII

Nina DNA ya Mungu. Ninafanya kazi za ajabu na kazi za kigeni kwa ujasiri. Mimi ni mvuna roho kwa mikakati ya kigeni!

**MAFUNZO ZAIDI**
Isaya 28:21 (NIV)

**MKAKATI WA BIBLIA WA SIKU 365 – SIKU YA 267**
Luka 18:18-43; Zaburi 100-102

GoodNews DAILY

# WA NJE YA DUNIA HII

**Wafilipi 3:20 (AMP)**
**Kwa maana sisi, [tuko tofauti kwa sababu] wenyeji wetu uko mbinguni…**

Kiumbe wa nje ya dunia hueleweka kwa kawaida kama kiumbe kutoka nje ya Dunia: mgeni kutoka sayari nyingine. Wakristo wanaweza kuelezewa kwa usahihi kama viumbe kutoka nje ya dunia. Sisi ni wageni Duniani, raia wa Mbinguni wanaoishi kwa muda miongoni mwa wale tulioitwa kuwapatanisha na Kristo.

Unapoishi katika nchi ya kigeni, unaweza kujifunza lugha na kuheshimu mila fulani za wenyeji, lakini uaminifu wako unabaki kwa nchi yako ya asili. Maadili yako, maamuzi yako, na hisia ya utambulisho hutoka huko. Unaweza kuonekana kama kila mtu mwingine, lakini wewe ni tofauti. Usemi wako, vipaumbele vyako, na majibu yako huonyesha mahali unapostahili kuwa.

Mashujaa wa imani walijulikana kama wageni duniani. Mtume Petro anatutambulisha kama wageni na wahamiaji. Dunia ni jukumu lako, si asili yako. Umepangiwa hapa tu. Mbinguni ni nyumbani kwako haswa; Dunia ni ziarani tu.

## MAOMBI YA LEO

Baba, uzuie moyo wangu usijiingize katika mifumo ya ulimwengu huu. Acha maisha yangu yaakisi wazi utamaduni wa Mbinguni ninakotoka na Mungu ninayemwakilisha.

## TAMKO LA KINABII

Mimi ni raia wa Mbinguni. Utii wangu ni kwa Kristo pekee. Ninabeba utamaduni wa Mbinguni na kutimiza majukumu yangu ya duniani bila kupoteza utambulisho wangu wa milele. Niko ulimwenguni, lakini si wa ulimwengu huu, katika Jina la Yesu.

**MAFUNZO ZAIDI**
Waebrania 11:13

**MKAKATI WA BIBLIA WA SIKU 365 – SIKU YA 268**
Isaya 41-42; Wafilipi 2

JUMAMOSI, SEPTEMBA 26



# MAFUTA SAFI

**Mhubiri 10:1 (RSUVDC)**
**Nzi waliokufa hufanya manukato ya mwuza marashi kutoa uvundo......**

Mwili wa mwanadamu hutoa na kupokea nishati kila mara. Sisi ni wasambazaji na wapokeaji, tukifanya kazi kama antena hai. Hii ndiyo sababu Maandiko hutoa maagizo wazi kuhusu mguso wa kimwili na kiroho. Mikono inapowekwa, upako huhamishwa kila wakati , iwe ni wa Mungu au la.

Kwa sababu usambaji huu ni jambo lisiloepukika, utambuzi ni muhimu. Biblia haisemi kuepuka uenezaji kabisa; inasema tusiruhusu ghafla . Lazima kuwe na uwazi uliothibitishwa wa chanzo. Kama mto, mafuta hutiririka kutoka kichwani kwenda chini. Ikiwa kichwa kimechafuliwa, kila kitu chini ya mto huathirika; na haihitajiki vingi kuchafua kile ambacho hapo awali kilikuwa safi.

Chochote chenye vichwa zaidi ya kimoja ni jitu. Mkanganyiko wa kiroho hutokana na kupokea sauti nyingi sana. Mungu hutoa sauti moja kuu, kichwa kimoja, chanzo kimoja cha ufunuo ambapo mafuta yako hutiririka. Katika Mwaka huu wa Mafuta Ajabu, fikiria kwa makini kuhusu mikono, maneno, na roho ya nani unapokea kutoka kwake. Linda mafuta yako.

## MAOMBI YA LEO

Baba, nipe utambuzi wa kutambua sauti uliyoituma kwa ajili yangu ili nipokee tu kile kinachotoka kwako.

## TAMKO LA KINABII

Mafuta yangu ni safi. Ninapokea kutoka chanzo ambacho Mungu amenipa. Ninaamuru na kutangaza kwamba hakutakuwa na nzi katika mafuta yangu.

**MAFUNZO ZAIDI**
1 Timotheo 5:22

**MKAKATI WA BIBLIA WA SIKU 365 – SIKU YA 269**
Isaya 43-44; Wafilipi 3

JUMAPILI, SEPTEMBA 27




# ISIYOFUNGIKA NIRA

**Isaya 10:27**
**...Nayo nira itaharibiwa kwa sababu ya kutiwa mafuta.**

Wengi wamefundishwa kwamba andiko hili linamaanisha kwamba upako utavunja nira baada ya kuwa juu ya mtu. Hata hivyo, hii inapunguza uzito kamili wa mstari huo. Upako unaozungumziwa hapa si tu wa kiutendaji; una nguvu ya kutosha kufanya nira isiweze kukugusa hata kidogo.

Fikiria tofauti kati ya matengenezo na kinga. Je, ungependa nira iwekwe juu yako kisha ikavunjwa, au ungependa uwe salama? Ulinganisho huo ni sawa na uponyaji dhidi ya afya ya Ki-Mungu. Uponyaji hurejesha kilichohabiwa na ugonjwa, lakini afya ya Ki-Mungu huzuia ugonjwa kukuvamia hata kabla. Moja ni nzuri; nyingine ni bora zaidi.

Wakati upako upo na unafanya kazi, ukandamizaji hauwezi kutulia, kikomo hakiwezi kujifunga, na mizigo haiwezi kujishikilia. Mafuta haya ya Ajabu huunda mazingira ambapo nira haziwezi kuishi. Mara tu zinapojaribu kukugusa, zinaharibiwa.

## MAOMBI YA LEO

Baba, asante kwa kuweka mazingira yanayozunguka maisha yangu ambapo ukandamizaji, vikwazo, na mizigo haviwezi kupumzika au kurudi. Acha upako huu utawale katika kila eneo la maisha yangu.

## TAMKO LA KINABII

Mimi sifungiki nira. Kwa upako huu wa ajabu, hakuna mzigo, kizuizi, au ukandamizaji unaoweza kunishikilia kwa Jina la Yesu.

**MAFUNZO ZAIDI**
Wagalatia 5:1 (KJV)

**MKAKATI WA BIBLIA WA SIKU 365 – SIKU YA 270**
Isaya 45-46; Wafilipi 4



# USHINDI USIOKUTOA JASHO

**Yoshua 10:11**
**Kisha ikawa ... ndipo BWANA alipowatupia mawe makubwa kutoka mbinguni...... hao waliokufa kwa kwa kuuwawa na hayo mawe ya barafu walikuwa ni wengi kuliko hao waliouawa na wana wa Israeli kwa upanga.**

Maandiko ya leo yanarekodi vita ambapo maadui wengi zaidi walikufa kutokana na mawe ya mvua ya mawe yaliyotumwa na Mungu kuliko kwa upanga wa Israeli. Matokeo hayakuwa matokeo ya ustadi, mkakati, au nguvu za juu za wanaume hao hodari, bali ya uingiliaji kati wa Mungu.

Kuna nyakati ambapo Mungu hataki kukupa nguvu za kupigana tu. Anataka ijulikane kwamba Yeye mwenyewe aliingia kwenye pambano kama mpiganaji. Ni kazi ya kigeni . Mwaka huu, Mungu anataka iwe wazi kabisa kwamba ushindi haupatikani kwa juhudi zako. Vita havijakabidhiwa kwako tena; Mungu anapigana moja kwa moja kwa ajili yako ili hakuna mtu anayeweza kujipatia sifa.

Katika msimu huu, usipime ushindi kwa kiasi cha juhudi unazotumia. Tazama mkono wa Mungu ukifanya kile ambacho Yeye pekee anaweza kufanya kwa njia ambazo haziachi shaka kwamba Yeye pekee ndiye aliyehakikisha matokeo.

## MAOMBI YA LEO

Baba, asante kwa kunipigania na kunipa ushindi wangu. Acha matokeo yathibitishe kwamba ilikuwa mkono wako pekee.

## TAMKO LA KINABII

Mungu mwenyewe ananipigania, na ushindi hauwezi kupingwa. Adui zangu watakuwa na uadui wao kwa wao. Nitashuhudia!

**MAFUNZO ZAIDI**
2 Mambo ya Nyakati 20:15

**MKAKATI WA BIBLIA WA SIKU 365 – SIKU YA 271**
Isaya 47-49; Wakolosai 1

JUMANNE, SEPTEMBA 29



# MAADUI WENYE AMANI

**Mithali 16:7**
**Njia za mtu zikimpendeza BWANA, hata adui zake huwapatanisha naye.**

Katika Mwaka huu wa Mafuta ya Ajabu, Mungu amekupa amani na adui zako kupitia vitisho vitakatifu. Hakuna mazungumzo yanayohitajika. Mungu anasuluhisha mambo kabla hujafika. Ni kama kutarajia vita vya kisheria virefu, na kisha kumkuta jaji tayari amekupendelea muda mrefu kabla ya miguu yako kugusa ngazi za mahakama. Hutaingia kushindana, bali kukusanya.

Songa mbele kwa ujasiri katika kipindi chote kilichobaki cha mwaka huu ukijua kwamba Mungu tayari amekutangulia na kukusafisha njia ya kutembea kwa amani. Furahi ukijua kwamba adui zako watakuwa marafiki zako mwaka huu. Haitakuwa kwa sababu wanakupenda au mioyo yao imebadilika, bali kwa sababu wanakuogopa. Wale waliokupinga hapo awali watajizuia sasa, kwa sababu watajua kwamba kushindana nawe kuna hatari. Haleluya!

## MAOMBI YA LEO

Baba, asante kwa kushindana na wale wanaoshindana nami. Kwa sababu yako, nitatembea kwa amani.

## TAMKO LA KINABII

Kila adui atatetemeka akiniona, litakapotajwa tu jina langu. Hakutakuwa na upinzani, kwa maana Mungu yuko pamoja nami. Mikataba inakuja. Pesa inakuja. Hakuna mtu atakayesimama dhidi yangu!

**MAFUNZO ZAIDI**
Zaburi 2:1-5

**MKAKATI WA BIBLIA WA SIKU 365 – SIKU YA 272**
Isaya 50-52; Wakolosai 2




# KIONDOA MAKUNYANZI

**Mwanzo 18:14**
**Kuna neno gani lililo gumu la kumshinda BWANA? ...**

Biblia inatuambia kuhusu Sara ambaye alikuwa na umri wa miaka sitini na mitano wakati wana wa Farao walipomtazama na kusema, “Mama Mia! ” Sitini na tano! Wakati, umri, na biolojia havikuwa na nguvu ya kufifisha mvuto wake. Makunyanzi hayakupatikana popote.

Vipi kuhusu Esta? Kulingana na nyakati, alikuwa na umri wa miaka tisini na tano hadi mia moja na kumi na tano alipoletwa katika jumba la mfalme Ahasuero. Lakini Biblia inasema alishindana na wasichana wadogo na akashinda! Esta mzee aliweka vitu vyake pembeni, na mfalme akasema, “ Huyo ndiye ninayempenda. ”

Usifanye kosa la kufikiri nazungumza na wanawake tu hapa. Ninakutangazia kwamba “makunyanzi” ya kimwili, kihistoria, na kifedha hayatakuondoa kwenye kile Mungu anachofanya mwaka huu. Makunyanzi ya zamani zako hayatakuzuia. Kile kilichoonekana kuwa kimeisha muda wake kitakuwa cha kipekee. Kile ambacho kingekufanya usiwe na sifa kitapuuzwa. Bwana anafanya kazi yake ya ajabu !

## MAOMBI YA LEO

Baba, asante kwa kufanya kile ambacho peke yako ndiye unayeweza kufanya. Acha kila ishara ya kuchelewa, kukwama, na kutostahili ifutwe na kazi Yako ya ajabu maishani mwangu.

## TAMKO LA KINABII

Kuchelewa kumekwisha! Wakati wangu umekombolewa, na kila kasoro za maisha yangu ya zamani zimeondolewa. Kile kilichonifanya nisistahili kimegeuzwa na kazi ya ajabu ya Mungu. Haleluya!

**MAFUNZO ZAIDI**
Mwanzo 12:9-15;
Esta 2:7-17

**MKAKATI WA BIBLIA WA SIKU 365 – SIKU YA 273**
Isaya 53-55; Wakolosai 3




# MWONGOZO WAKO WA KINABII WA KILA SIKU

Gazeti la Habari Njema Kila Siku linafurahi kutambulisha matoleo mahususi yaliyoundwa kwa uangalifu kwa ajili ya vijana na watoto, yakiandamana na ibada yetu kuu. Kila toleo hutoa Neno la kinabii la kila siku moja kwa moja kutoka moyoni mwa Nabii Uebert Angel, lililowasilishwa kwa njia ambayo inazungumza na kila hatua ya maisha na kuunganishwa na kila mwanafamilia.

Ibada hizi zimewekwa pamoja kwa uangalifu ili kufanya Neno la Mungu liwe hai kwa njia inayohusiana na yenye matokeo, kusaidia wasomaji kukua katika imani, ufahamu na ukomavu wa kiroho. Dhamira yetu ni kuhakikisha kwamba ukweli wa Mungu unafikia mioyo ya vizazi vyote, na kutia moyo kutembea Naye kwa kina kila siku.




**TOLEO LA VIJANA**

Huingia ndani zaidi na maarifa yenye nguvu ambayo huwapa vijana kukabiliana na changamoto za maisha kwa hekima na nguvu za kiroho.

**TOLEO LA WATOTO**

Imeundwa ili kutambulisha dhana za msingi za imani, upendo, na ahadi za Mungu kwa njia ya kufurahisha na ya kuvutia ikisaidia mioyo michanga kusitawisha uhusiano thabiti na Mungu na kuifanya Biblia iwe hai.

Kila siku, utapokea Neno lako la Kinabii la Siku lililoandikwa na Nabii Uebert Angel, ujumbe wa kiungu wa kuimarisha kutembea kwako na Mungu na kukuongoza katika kuishi kwa Neno lake. Ni njia yenye nguvu kwa familia kukua pamoja katika imani na kuimarisha uelewa wao wa ukweli wa Mungu.

**USIKOSE!**
Anza kufurahia nguvu ya mabadiliko ya GoodNews Daily, mwongozo wa kinabii ulioundwa kuinua na kutia moyo kila kizazi!

SCAN ME



BWANA WETU

# YESU KRISTO

Bwana wetu Yesu Kristo ndiye msingi wa imani ya Kikristo, maisha yake na mafundisho yake yameathiri sana mwendo wa historia. Bwana wetu Yesu Kristo anajulikana kwa huruma yake isiyo na kifani, hekima, na matendo ya miujiza Aliyofanya. Ujumbe wake ulijikita katika upendo, msamaha, na ahadi ya uzima wa milele, ukitoa tumaini na ukombozi kwa wote wanaomwamini. Katika huduma Yake yote, Alisafiri katika nchi za Yudea, akiponya wagonjwa, akiwafariji walioteseka, na kufundisha kuhusu ufalme wa milele wa Mungu.

Kumpokea Yesu Kristo kama Bwana na Mwokozi wako binafsi kunamaanisha kukubali mafundisho Yake na kualika uwepo Wake wa mabadiliko maishani mwako. Ni safari ya kuelekea utimilifu wa kiroho, yenye msingi katika imani, upendo, na ahadi ya wokovu.

Kupitia Bwana wetu Yesu Kristo, tunapata nguvu, tumaini, na njia ya amani ya milele. Kufanywa kuwa mkamilifu, au kuokolewa, ni kujisalimisha kwa Mungu na mpango wake na kusudi lake kwa maisha yetu. Ni kugeuka kutoka kwenye njia zetu za zamani na kumgeukia Yesu Kristo, kumwomba msamaha kutoka kwenye dhambi zetu na kutupa maisha mapya ndani yake.

**WARUMI 10:9**
**“Ukikiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka.”**

Wokovu ni zawadi ya bure ya Mungu kwetu na tunakuwa watoto Wake. Ni kibali kisichoweza kubatilishwa katika familia ya Mungu na ni uwezeshaji wa kuishi maisha kikamilifu na kikamilifu kwa kusudi la kumwakisi Mungu kwa uumbaji Wake wote.



## JE, UMEMPOKEA

# YESU KRISTO?

**"Kwa maana Mwana wa Adamu alikuja kutafuta na kuokoa kile kilichopotea." - Luka 19:10**

**TUNAWAKARIBISHA KUMFANYA YESU KRISTO, BWANA WA MAISHA YAKO KWA KUOMBA SALA HII:**

"Ee Bwana Mungu, ninakuja kwako katika jina la Yesu Kristo. Ninaamini kwa moyo wangu wote katika Yesu Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai. Ninaamini kwamba alikufa kwa ajili yangu na Mungu alimfufua kutoka kwa wafu. Ninaamini yu hai leo. Ninakiri kwa kinywa changu kwamba Yesu Kristo ndiye Bwana wa maisha yangu tangu siku hii. Kupitia Yeye na kwa jina Lake, nina uzima wa milele; nimezaliwa mara ya pili."

Asante Bwana, kwa kuokoa roho yangu!
Sasa mimi ni mtoto wa Mungu. Haleluya!"

**Hongera! Sasa wewe ni mtoto wa Mungu.**

**Endelea kukua kwa kukaa katika Neno Lake, kuomba kila siku, na kuweka imani yako kuwa imara. Mungu ana safari ya ajabu mbele yako.**

**Ili kukua zaidi kama Mkristo wasiliana nasi:**
**UK:** +44 1244 727242 | **USA** +1 448 877 0344
**RSA:** +27 872 654 913 | **ZWE** +263 8677 211 645
**WhatsApp:** 0773 195 955
**Email: gnd@goodnewsworld.com**

SCAN ME



KIFUNGU CHA MAANDIKO YA

# ULINZI

**Umezungukwa na Nguvu za Mungu, Hakuna Ubaya Unaoweza Kusimama Juu Yako!**

**ISAYA 54.**

**14.** Nimejenga imara, niliyowekwa katika haki. Mbali na shida yoyote, hakuna cha kuogopa! Mbali na hofu, hata haitakuja karibu!

**15.** Mtu akinishambulia, sitafikiri hata kidogo kuwa Mungu ndiye aliyemtuma. Na ikiwa yeyote atanishambulia, hakuna kitakachotokea.

**16.** Mungu alimuumba mhunzi ateketeze mfua chuma chake na kutengeneza silaha iliyoundwa kuua. Pia amemuumba mharibifu.

**17.** Lakini hakuna silaha inayoweza kunidhuru iliyowahi kughushiwa. Yeyote anayenituhumu ataondolewa kuwa mwongo. Mimi ni mtumishi wa Mungu hivyo ndivyo ninavyoweza kutarajia Mungu atahakikisha kwamba kila kitu kinaenda vyema kwa ajili yangu.

**Hivi ndivyo Mungu anasema na haitashindwa katika jina la Yesu!**

**Ili kukua zaidi kama Mkristo wasiliana nasi:**
**UK:** +44 1244 727242 | **USA** +1 448 877 0344
**RSA:** +27 872 654 913 | **ZWE** +263 8677 211 645
**WhatsApp:** 0773 195 955
**Email: gnd@goodnewsworld.com**

SCAN ME

GoodNews DAILY



# DIRA YA DUNIA INAHITAJI BAJETI YA ULIMWENGU

**KUWA MPENZI WA GOODNEWS KILA SIKU**




Kila mwezi, washirika wetu waliojitolea husambaza nakala za ibada ya GoodNews Daily bila malipo kwa watu katika vituo vya watoto yatima, magereza, hospitali, nyumba za wazee, shule, taasisi za serikali na maeneo mengine mengi duniani kote. Tumepokea shuhuda nyingi za wokovu, uponyaji, utoaji wa kimungu, na miujiza mingine mingi kama matokeo ya kampeni hii ya kimataifa ya usambazaji.

Jiunge nasi na uwe sehemu ya harakati hii tukufu ya Mungu, ukimpa mtu mabadiliko ya mwanzo mpya na matumaini mapya ya kesho.

**Ili kukua zaidi kama Mkristo wasiliana nasi:**
**UK:** +44 1244 727242 | **USA** +1 448 877 0344
**RSA:** +27 872 654 913 | **ZWE** +263 8677 211 645
**WhatsApp:** 0773 195 955
**Email: gnd@goodnewsworld.com**

SCAN ME

GoodNews DAILY



## UJUMBE MMOJA

# LUGHA NYINGI

**KWA SABABU UJUMBE WA KRISTO HAUJUI KIZUIZI CHA LUGHA**

Gazeti la Habari Njema Kila siku linabadilisha maisha duniani kote kupitia tafsiri katika lugha nyingi zinazozungumzwa na watu wengi, na hivyo kuwapa mamilioni ya watu uwezo wa kupata maarifa ya kuokoa ya Yesu Kristo. Kote katika mataifa na tamaduni, watu kila mahali wanakutana na Neno la kinabii na kupata uzoefu wa kubadilisha maisha na Mungu kupitia ibada hii.




Gazeti la Habari Njema KIla siku linavunja vizuizi na kuzungumza moja kwa moja ndani ya mioyo ya watu katika lugha yao wenyewe. Kuanzia majumbani na shuleni hadi makanisani, vyuo vikuu na hata miongoni mwa viongozi na marais, inafikia kila ngazi ya jamii.

Kwa kubeba Neno la kinabii la Nabii Uebert Angel kwa kila taifa na kila lugha, GoodNews Daily inasaidia kutimiza Agizo Kuu katika kizazi hiki.

**ILI KUDHAMINI TEMBELEA TOVUTI YETU:**

**www.goodnewsdailydevotional.com**

GoodNews DAILY

## KARIBU
# MTANDAONI KWETU




**KUJUA ZAIDI TEMBELEA TOVUTI YETU LEO**

Tembelea tovuti ya GoodNews Daily ili kupata ibada za watu wazima, vijana, na watoto, kila moja iliyoandikwa kwa uangalifu ili kuimarisha imani yako na kuongeza uelewa wako wa Neno la Mungu. Tovuti hii pia ina mafundisho ya utambuzi kutoka kwa Nabii Uebert Angel, masasisho kuhusu matukio ya hivi punde ya GoodNews Daily, na nyenzo mbalimbali zilizoundwa kukusaidia kukua na kustawi katika kila eneo la maisha yako.

Iwe unatafuta maongozi ya kila siku, ufunuo wa kina, au njia za kuendelea kuwasiliana na Ulimwengu wa Habari Njema, kila kitu unachohitaji kinapatikana katika sehemu moja kwenye tovuti ya GoodNews Daily.

**Ungana nasi kwenye mitandao ya kijamii:**
@goodnewsdailydevotional

**TOLEO 3 | 2026**

**JULAI- AGOSTI- SEPT**

---

Habari Njema Kila Siku inatengenezwa na Spirit Embassy:
Kanisa la GoodNews, likishiriki mafundisho ya kinabii na ufunuo wa Nabii Uebert Angel. Imejitolea kueneza ujumbe wa Yesu Kristo na kuwatia nguvu waumini kwa Neno la Mungu.

**KWA HABARI ZAIDI, MAOMBI, AU ILI KUHUSISHWA, TAFADHALI WASILIANA NA TAWI LAKO**

Jina la Tawi:
Mtu wa Mawasiliano:
Nambari ya Simu:
Barua pepe:
Anwani:

**Hakimiliki © 2025 na Uebert Angel**
**Haki zote zimehifadhiwa.**

support@goodnewsworld.com
www.goodnewsworld.com

Kwa habari zaidi au kushiriki ushuhuda wako:
gnd@goodnewsworld.com | www.goodnewsdailydevotional.com

**Ili kukua zaidi kama Mkristo wasiliana nasi:**

**UK:** +44 3333 448 612 | **USA** +1 240 781 6942
**RSA:** +27 51 004 0209 | **ZWE** +263 773 195 955
**Email:** gnd@goodnewsworld.com

SCAN ME




FKwa mawasiliano zaidi ya jinsi ya kukuwa kama mkristo, wasiliana nasi katika:

UK: +44 3333 448 612
USA: +1 240 781 6942
RSA: +27 51 004 0209
ZWE: +263 773 195 9555

gnd@goodnewsworld.com
goodnewsdailydevotional.com

SKANI KUPAKUWA BURE